**CHINA** yaipa Tanzania mabilioni kutekeleza miradi ya maendeleo

UKURASA 4



**MWINYI:** Niliepuka kubishana, kumkosoa Nyerere hadharani

UKURASA 3


ama

AFYA NA MAZINGIRA

DK. LEONARD MABAI:

**Mwanza tunakikabili hivi kichocho, ugonjwa 'pasua kichwa' Kanda Ziwa**

• Kimyakimya imefikia milioni 22 nchini

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Mei 13, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580579

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# Watu wote kupata huduma bima afya

UKURASA 2




Rais mstaafu Jakaya Kikwete (kushoto), akipokeza zawadi ya mswala kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake na wadau jijini Dar es Salaam juzi jioni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## REPOA yamwonyesha Samia mambo manne ya maendeleo

UKURASA 2



Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari



UKUAJI WA UCHUMI 8% - 10%

MAZINGIRA MAZURI YA UWEKEZAJI

NGUVU KAZI YA VIJANA

KILIMO CHA KISASA

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MWANAJESHI MBARONI MADAI YA KUSAFIRISHA WAHAMIAJI

JESHI la Polisi mkoani Tanga linawashikilia watu saba raia wa Bangladesh, kwa tuhuma za kuingia nchini bila kibali. madeni...

UKURASA WA 4

### BUNGE LATAKA AJIRA ISIZINGATIE NIDA BAADHI YA MAENEO

BUNGE limeishauri serikali kuondoa kigezo cha ulazima wa namba ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kwenye maombi ...

UKURASA WA 5

### MAHINDI YA TANZANIA YAANZA KUINGIA KENYA

WIKI moja baada ya Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, kuruhusu mahindi ya Tanzania yaliyokuwa yamezuiliwa mipakani kuingia nchini humo, wafanyabiashara wameanza kupitisha shehena ya...

## Mkwamo malori bandarini watikisa Bunge

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA: TUTAISHANGAZA AFRIKA** UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

## HABARI KITAIFA

# Watu wote kupata huduma bima afya

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imesema inatarajia kupeleka bungeni muswada wa bima ya afya kwa wote ambao kabla utashirikisha wadau muhimu ikiwamo sekta binafsi kutatua changamoto zinazojitokeza.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge waliochangia katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendelea ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Naibu Waziri, Dk. Godwin Molel, alisema wengi walizungumzia bima ya afya kama kikwazo katika kupata huduma bora.

"Wakati wa kuleta muswada wa bima ya afya kwa wote tutahakikisha kuna kipengele kinachoruhusu sekta binafsi kushiriki kwenye bima," alisema na kuongeza:

"Tumezingatia kabla ya kuleta bima ya afya kwa wote bungeni wananchi washirikishwe, wadau wote kuanzia wananchi ambao itawagusa kabla ya muswada kuja bungeni, tunaamini nanyi (wabunge) mtaweka mchango ili kuondoa matatizo yaliyopo kwenye bima ya afya iliyopo sasa," alisema.

Aidha, Waziri huyo alikiri kuwapo kwa upungufu wa dawa na kusababisha wananchi wanaotumia bima ya afya kuhangaika na kutoona thamani ya kadi, huku baadhi ya maeneo wakisafiri umbali mrefu kufuata dawa katika maduka kwa kutumia nauli ya Sh. 10,000 kufuata dawa ya Sh. 3,000.

Naye Waziri wa Afya, Dk. Doroth Gwajima, alisema wameandaa utaratibu wa kuwa na wahudumu maalum wa wazee ambao watavaa fulana zilizoandikwa "Nakupenda Sana Mzee" ambao watawajibika moja kwa moja kwa kundi hilo. Wakichangia mjadala huo, kilio cha ukosefu wa dawa, matibabu bure kwa wazee, wajawazito na watoto kilitawala, huku wakitaka hatua kuchukuliwa kuokoa maisha ya wananchi. Watunga sheria hao walisema ukosefu wa wahudumu wa afya na wataalamu mbalimbali ni tatizo kubwa nchini, huku hakuna motisha kwa wafanyakazi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Regina Qwaray, alisema huduma ya mama na mtoto ni bure, lakini maeneo mengi bila fedha hawapati huduma, huku wengine wakitembea umbali wa zaidi ya kilomita 70.

Alisema huduma ya matibabu bure kwa wazee ni tatizo kubwa kiasi cha wengi kuteseka na kwamba ni muhimu kuchukua hatua kwa kuwa kila mmoja ni mzee mtarajiwa.

Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa (CCM), George Malima, alisema kutokana na ukosefu wa dawa wapo wauzaji wa maduka binafsi wanauza zilizopitwa na wakati jambo ambalo ni hatari kwa afya za watumiaji na kutaka serikali kufanya uchunguzi wa kina.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Mariki, alisema mkoa wa Katavi kuna upungufu wa watumishi ni asilimia 72 waliopo ni asilimia 28, upungufu wa vifaa tiba ni asilimia 60 vilivyopo ni asilimia 40.

Aidha, alisema huduma ya damu kwa wajawazito ni tatizo kubwa kwa kuwa wanatakiwa kulipia na wanapoleta ndugu wa kuwachangia wanatakiwa kununua mifuko ya kuhifadhia Sh. 16,000.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga, alisema katika Hospitali ya Tabora wajawazito wanatozwa Sh. 50,000 kujifungua mtoto wa kiume na Sh. 40,000 mtoto wa kike.

Mbunge wa Jimbo la Tarime (CCM), Michael Kiambati, alisema kilio kikubwa cha wananchi wake ni ukosefu wa dawa kwa kuwa ni kawaida kwenda hospitali, kituo cha afya na zahanati na kukosa dawa.

Alisema maeneo mengi hakuna zahanati kiasi cha wajawazito wengi kupoteza maisha na kujifungulia njiani, huku hospitali pekee ya Bomani ikielemewa kwa wagonjwa na haina madaktari na wahudumu wa afya wa kutosha.

Alisema kutokana na upungufu wa watumishi wagonjwa wanaojiweza wanalazimika kufanya usafi kabla ya kupata huduma, jambo ambalo siyo sahihi.

Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini (CCM), Maimuna Mtanda, alisema wazee, wajawazito na watoto wanateseka kwa kukosa huduma sahihi, licha ya kuahidiwa huduma bure za afya.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bahati Ndingo, alisema sera ya wazee ya mwaka 2013 haina sheria na kwamba ni muhimu serikali ikaeleza lini itaileta ili wapate huduma bila usumbufu.

# REPOA yamwonyesha Samia mambo manne ya maendeleo

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini nchini (REPOA), Dk. Donald Mmari, amemshauri, Rais Samia Suluhu Hassan, mambo manne ili nchi iweze kusonga mbele kimaendeleo.

Kwenye ushauri huo, Dk. Mmari alisema uchumi wa Tanzania unapaswa kukua kwa kasi angalau kiwango cha chini kifikie asilimia nane au kifike asilimia 10 na kuendelea, hali ambayo itarahisisha kasi ya kupungua kwa umaskini.

Alitoa ushauri huo jana baada ya kutembelea Kampuni ya The Guardian, inayozalisha magazeti ya The Guardian, Nipashe na Nipashe Jumapili, kuona namna uzalishaji wa magazeti unavyofanyika.

Akizungumza kwenye ziara hiyo, Dk. Mmari alisema tafsiri ya uchumi kukua kwa kasi maana yake ni shughuli za kiuchumi zinaongezeka na wananchi waliowengi wanakuwa wanashirikishwa.



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari (katikati), alipotembelea katika chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni Viwandani, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja wa Sheria na Raslimali Watu wa TGL, Emmanuel Matondo (kulia), Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (wa pili kulia) na Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa REPOA, Godfrey Kalagho. **PICHA: JOHN BADI**

Dk. Mmari alisema: "Utaona uzalishaji viwandani, mashambani unaongezeka kwa hiyo hata mapato nayo yanaongezeka, ajira zinaongezeka na sekta za umuhimu na msingi mfano uchukuzi, ujenzi, biashara zinachangia kwenye kukua kwa pato la taifa."

Dk. Mmari alisema kasi ya ukuaji wa uchumi inatakiwa ianzie asilimia nane na kuendelea.

Jambo la pili, alishauri serikali kuhakikisha kunakuwapo na uwekezaji wa ndani na nje ya nchi, akibainisha kwamba nchi yoyote haiwezi kuwa na uchumi imara pasipo kuwa na uwekezaji thabiti.

Dk. Mmari alisema ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) muundo wake una matumizi ya kaya, matumizi ya serikali, uwekezaji, jumla ya mauzo ya nje na kutoa manunuzi kutoka nje.

Alibainisha kuwa ili uweze kukua kiuchumi, lazima kuwapo na uwekezaji mkubwa ambao utatengeneza ajira na kuwezesha sekta nyingine kuchangamka na serikali kupata mapato zaidi.

"Mapato yakiongezeka kwa hiyo mishahara itaongezeka, miundombinu, huduma za wananchi. Unaupataje uwekezaji, lazima kuwe na mazingira na biashara lazima yawe rafiki," alisema Dk. Mmari na kuongeza:

"Tukiongelea mifumo ya kodi, Rais wetu ametoa maelekezo kuangalia taasisi zinazosimamia uwekezaji, biashara ziwe zinasimamia na kuwezesha badala ya kuwa vikwazo."

Alitaja jambo la tatu ni nguvu kazi ya vijana, kwamba Tanzania na nchi zinginezo zinazolingana kiuchumi wanategemea nguvu kazi izalishe kwa sababu hazina mitaji wala teknolojia kubwa.

Alisema hivyo zinahitaji uzalishaji kupitia rasilimali watu iliyonayo.

"Tukiangalia muundo wa idadi ya watu utaona tuna asilimia kubwa ya vijana, watoto chini ya umri wa miaka 15 ni takribani asilimia 44, hivi karibuni wanaingia kuungana na nguvu kazi kuungana na asilimia nyingine takribani 30 ya watu kati ya miaka 15 mpaka 65," alisema Dk. Mmnari na kuongeza:

"Lazima wajengewe uwezo hawa vijana, maarifa na ujuzi wa kuzalisha ili kusudi waongeze pato la taifa, sasa hii nguvu kazi ikipotea ikawa tegemezi, uchumi hauwezi kukua, lazima tuangalie eneo hili la uwekezaji na nguvu kazi ya vijana."

Jambo la nne, alishauri serikali iwekeze kwenye kilimo cha kisasa cha kuchakata mazao.

Akizungumzia miaka 25 ya REPOA iliyotimia mwaka jana tangu kuanzishwa kwake, alisema pamoja na kwamba walishindwa kuisherehekea kutokana na uwapo wa ugonjwa wa corona lakini wanajivunia kuwajengea uwezo watafiti wengi kwa kutumia mafunzo na namna ya kufanya utafiti bora wa masuala ya kisera.

Alisema REPOA imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya watafiti wachanga ambao hujifunza kwa kufanya utafiti na wamenufaika.

Alisema kati ya watafiti hao wapo wanaofanya kazi serikalini idara za mipango, taasisi za kimataifa na wengine wamebaki kuwa watafiti wa kujitegemea.

Kuhusu malalamiko ya hali ya umaskini huku uchumi ukionekana umekua, Dk. Mmari alisema upunguaji wa umaskini unategemea mambo mengi, lakini makubwa ni ukuaji wa uchumi ili kipato cha mtu mmoja mmoja kikue.

Kuhusu ziara hiyo, Dk. Mmari alisema Kampuni ya The Guardian Ltd ni moja ya wadau wao kwa sababu kazi za utafiti wanazozifanya, matokeo hutakiwa kuwafikia watu mbalimbali ikiwamo kupitia vyombo vya habari.

Kadhalika, Dk. Mmari alimkabidhi Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, vitabu mbalimbali vya utafiti uliofanywa na REPOA walioufanya, ambaye naye aliahidi kuvifanyia kazi.

# Giga, Zungu warejea kuliongoza Bunge

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE jana liliwapitisha wenyeviti watatu wa Bunge kwa ajili ya kumsaidia Spika kuongoza vikao.

Waliopitishwa ni Mbunge wa Ilala, Mussa Zungu, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga, pamoja na Mbunge wa Mufindi Kusini, David Kihenzile, ambaye anashika nafasi hiyo kwa mara ya kwanza.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, jana aliwasilisha majina yao bungeni kwa ajili ya Bunge kuwachagua, hata hivyo kutokana na idadi ya wagombea kuwa watatu na nafasi zilizopo ni tatu, Bunge liliwathibitisha.

Akitoa maelezo, Dk. Tulia alisema kanuni ya saba ya Kanuni za Bunge imeweka uwapo wa wenyeviti watatu wa bunge ambao watamsaidia Spika kuongoza vikao kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika.

Naibu Spika huyo alisema wenyeviti hao wamepita bila kupingwa, kwamba utaratibu kama huo ulitumika katika Bunge la 11.

Akizungumza baada ya kupitishwa na Bunge, Zungu alisema kazi hiyo itakuwa nyepesi kama wabunge watakuwa na ushirikiano.

Naye Giga alishukuru kwa kuaminiwa na wabunge na kuahidi kuendelea kuwa mwadilifu.

Kwa upande wake, Kihenzile aliahidi kutoa ushirikiano mzuri kwa wabunge na kuwa msaidizi wa Spika mwaminifu.

HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza jambo na kumpongeza Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, baada ya kuapishwa kuliongoza tena taifa hilo, katika Uwanja wa Kololo, jijini Kampala, nchini Uganda jana. **PICHA: IKULU**

# Mkwamo malori bandarini watikisa Bunge, PM aagiza

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE jana liliahirisha shughuli zake kwa dakika 20, ili kujadili suala la mkwamo wa malori katika Bandari ya Dar es Salaam, huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akilazimika kufanya ziara ya ghafla bandarini na kutoa maagizo.

Wakati mjadala wa foleni ya malori kuingia kuchukua mizigo bandarini ukiendelea bungeni, Waziri wa Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Jenista Mhagama, aliingilia kati na kusema serikali inafahamu na imeshaanza kulishughulikia na kwamba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameenda bandarini na kuhakikisha yanayojiri serikali inatekeleza wajibu wake ili uendeshaji urudi kawaida.

"Nawaomba sana wabunge watupe nafasi, tayari Waziri Mkuu ameshaenda na taarifa itatolewa, akishakamilisha wataona hatua zilizochukuliwa na serikali," alisema.

Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alichangia kwa kuwataka wabunge kuipa muda serikali kufuatilia hadi Jumatatu na kama hakutakuwa na mabadiliko Bunge litaamua.

### WAZIRI MKUU BANDARINI

Akiwa bandarini hapo, Waziri Mkuu aliitaka Mamlaka ya Bandari nchini (TPA) pamoja na Mamlaka ya Mapato (TRA) kurekebisha mifumo yao ili kuharakisha upakuaji mizigo.

Waziri Mkuu alisema Bandari ya Dar es Salaam ndiyo taswira ya uchumi wa nchini, hivyo ni lazima kulindwa kwa nguvu zote.

"Malalamiko yote hata kule nje yanazungumzia mfumo wenu TRA bado haufanyi kazi yake vizuri na kwa kutofanya kazi vizuri unawakwaza hawa wadau wawili bandari pamoja na kitengo cha Ticts wateja wetu wanahangaika mno," alisema Majaliwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eric Hamisi pamoja na kukiri kuwapo kwa changamoto mbalimbali ikiwamo urekebishaji wa miundombinu ya barabara, lakini alisema si kweli kuwa malori ya mizigo yanachukua muda wa siku tatu kushusha mzigo, bali mizigo yote hushushwa ndani ya saa 24.

Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alikiri kuwapo kwa changamoto katika mfumo wa Tancis ambayo inasababishwa na vifaa na suala la mtandao, kwamba aliahidi kulishughulikia.

### ILIVYOKUWA BUNGENI

Awali, wabunge walichangia hoja iliyowasilishwa na Mbunge wa Mafinga, Cosato Chumi, kutaka Bunge kujadili suala hilo kwa kuwa shughuli za uchumi zimesimama kutokana na bandari hiyo kutokufanya kazi.

Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), alisema huduma za bandari Dar es Salaam, zinasikitisha licha ya kuwa ni ng'ombe wa maziwa wa nchi, ambaye akitunzwa na kukamuliwa vizuri uchumi wa nchi ungezidi kukua, lakini sasa watu wanakimbilia bandari za Beyra kutokana na uzembe.

Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndayisaba Luhoro, alisema uchumi wa Ngara unategemea Bandari ya Dar es Salaam kwenye miji ya Kabanda, Rusumo na Benako kwa madereva kuegesha magari na kulala, kula na shughuli nyingi zinazoacha fedha katika mji huo.

"Kuchelewa kunaathiri uchumi wa wananchi wa Ngara, serikali ifanye haraka kushughulikia changamoto iliyopo bandarini ili wasikose fedha, kitendo cha Bandari kutofanya kazi siku mbili hadi tatu kinaathiri uchumi wa Watanzania," alisema.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, alisema fedha nyingi imewekezwa Bandari, lakini sasa kuna ucheleweshaji wa utoaji na uingizaji wa mizigo jambo ambalo linadhihirisha fedha iliyowekezwa haitarudi, wateja watakimbilia bandari nyingine licha ya Dar es Salaam kuwa katika eneo zuri kijiografia. Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisema serikali ifanye uchunguzi kama kuna hujuma dhidi ya uchumi, huku akitaka uchunguzi wa kina kwa kuwa mapato ya siku tatu kupotea siyo kitu kidogo.

Mbunge wa Jimbo la Mlimba (CCM), Godwin Kunambi, alisema tatizo kubwa ni kukosekana kwa uzalendo na kwenye taasisi yoyote ili ifanye vizuri lazima kiongozi wa juu awe mzuri na kama kuna rushwa au uozo wowote ni lazima hatua zichukuliwe dhidi ya kiongozi.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko, alisema kwa yanayoendelea bandarini hakuna nchi itakuja Tanzania kama mzigo unakaa wiki nzima, hali hiyo inasababisha kupandisha gharama ya bidhaa huku akitoa mfano wa saruji nyeupe jijini Dodoma ilipanda kutoka Sh. 25,000 hadi 50,000.

Mbunge wa Maswa Mashariki (CCM), Stanslaus Nyongo, alisema gharama ya kuchelewa kushusha na kupakia ni kubwa, Bandari ya Dar es Salaam, inategemewa na nchi zaidi ya nane na kwamba kuna wakati gharama ziliongezwa watu wa nchi ya Congo wakakimbilia Bandari ya Beyra, na nchi nyingine zitakimbia kama hali hiyo haitashughulikiwa.

Alisema kuna shida kubwa kwenye 'flow meter' huku akieleza kwa mwaka bandari hiyo ina uwezo wa kushusha mizigo tani milioni 17, lakini inayoshushwa ni chini ya milioni nne.

Mbunge wa Ilala (CCM), Mussa Zungu, alisema tatizo linatokana na bandari kuhama kutoka katika mfumo wa zamani ambao ilikuwa rahisi na kwenda mpya ambao siyo rafiki katika utoaji na kuingiza mizigo.

# Mwinyi: Niliepuka kubishana, kumkosoa Nyerere hadharani

**Na Sanula Athanas**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Nwinyi, amebainisha kuwa wakati wa uongozi wake, aliepuka kubishana hadharani na mtangulizi wake, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, akiwaonya viongozi wa sasa kujaribu kupata uhalali wa wanayoyafanya kwa kutupia lawama viongozi waliopita.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema aliona ilikuwa muhimu kwake kuepuka kubishana na Mwalimu Nyerere hadharani wala kukosoa uamuzi na yote yaliyofanyika wakati wa uongozi wake. "Ipo hulka ya kibinadamu ya viongozi wapya kujaribu kupata uhalali wa wanayoyafanya kwa kutupa kila aina ya lawama kwa viongozi waliopita. Hayo, kwa maoni yangu ni makosa makubwa. "Hakuna kitu rahisi kama kukosoa wengine, lakini wananchi hawachagui kiongozi ili akaorodheshe lawama. Ukichaguliwa na wenzako kuwaongoza unakuwa umepewa dhamana kubwa kupeleka taifa mbele.

"Wananchi wanataka kuona matokeo chanya ya unachokifanya wewe uliye na serikali kwa wakati huo, wakitambua kuwa kila awamu ya uongozi ina nafasi yake na inachokifanya ni sehemu ya mradi usioisha wa ujenzi wa nchi na kutumikia wananchi," anasihi. Mwinyi anafafanua kuwa mageuzi mengi yaliyofanyika wakati wa awamu yake hayakuwa ya kutafuta umaarufu, bali kuwaondolea wananchi adha mbalimbali.

"Hatukuandika waraka, hatukubuni itikadi mpya na wala hatukutumia majukwaa kujinasibu. Mengi tuliyafanya kimya kimya, kwa ujasiri lakini kwa hekima pia. "Na siku zote nilijitahidi kupata maoni na baraka za chama na kusikiliza na kupokea ushauri kwa dhati kabisa na kuuzingatia, si kutimiza wajibu tu.

"Kutoka kwa Mwalimu niliimarishwa hulka yangu ya kusikiliza kwa makini maoni na ushauri wa wengine kabla ya kufanya uamuzi na kuutekeleza. Na baada ya kuelewana na wenzangu tulisambaa nchi nzima kuwafahamisha wananchi," anasema.

Mwinyi anabainisha kikwazo kikubwa kilichomkumba wakati wa kufanya mageuzi hayo kilitokana na kundi analiloliita la uhafidhina ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), viongozi wenzake walioona vigumu kukubali haja na hoja ya mabadiliko, hasa pale ambapo hawakuwa na uhakika na msimamo wa Mwalimu Nyerere kuhusu mageuzi.

Katika kitabu chake hicho, Mwinyi pia anabainisha namna hali ya uchumi wa nchi ilivyokuwa mbaya wakati anakadhibiwa kijiti huku akisifu mchango wa Mwalimu Nyerere katika kurekebisha hali hiyo. Mwinyi anaweka wazi kuwa hata shinikizo IMF na Benki ya Dunia (WB) kwa Tanzania kukubaliana na masharti yao kama nchi inataka fedha (misaada na mikopo) kutoka kwao na wahisani wengine kutoka nchi za Magharibi, lilitatuliwa kwa ushauri wa Mwalimu Nyerere.

Anafafanua kuwa Mwalimu Nyerere hakukubaliana na baadhi ya masharti hayo na aliweka msimamo mkali na hivyo makubaliano hayakufikiwa mpaka anaondoka madarakani.

Katika kutatua suala hilo, Mwinyi anarejea ushauri wa Mwalimu Nyerere akimnukuu: "Tazameni, pesa bado tunazihitaji ili tukwamue uchumi wetu uende mbele. Hali ni mbaya kweli. Maadamu mimi nimeng'atuka, siko serikalini, huu ndiyo wakati mzuri wewe Sheikh Ali na timu yako mkamilishe mazungumzo hayo na ninaamini yatakwenda vizuri maana wakubwa hao wanajua kuwa yule mkorofi keshaondoka".

Mwinyi anasema ataendelea kumshukuru Mwalimu kwa uamuzi wake wa kuitisha kikao cha Kamati Kuu ya CCM (kilifanyika Zanzibar) na kutoa kauli ile mbele ya Kamati Kuu na hivyo kumpa rukhsa ya kuendelea na kazi hiyo ya kuimarisha uchumi wa nchi.

# Bunge lashauri ajira isizingatie NIDA baadhi ya maeneo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuondoa kigezo cha ulazima wa namba ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kwenye maombi ya ajira za afya na ualimu zilizotangazwa hivi karibuni kwa wilaya zisizo na ofisi ya mamlaka hiyo.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitoa kauli hiyo bungeni jana kufuatia mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Nkenge (CCM), Florent Kyombo wa kutaka Bunge lijadili suala hilo kutokana na kigezo hicho kinavyoweza kusababisha vijana kukosa ajira.

Akitoa majibu ya mwongozo huo, Dk. Tulia, alisema: "Waziri wa Mambo ya Ndani, afuatilie hayo maeneo nadhani tutawapa muda wao waangalie, kama kuna wilaya haina ofisi hicho kigezo kwasasa inabidi kiondolewe kwa sababu vijana watakosa fursa ya ajira, lakini kama wilaya inayo mwendelee na utaratibu na mtoe hizo namba kwa haraka."

Alisema kazi zilizotangazwa na serikali miongoni mwa kigezo ni kutaka namba za NIDA.

"Mtakumbuka kama miaka miwili hivi TCRA (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania), walikuwa wanasajili namba za simu na wakawa na uhitaji wa namba ya NIDA, awali walisema kitambulisho, baadaye wakasema namba na watu wengi walipata hizo namba sina hakika sana na ukubwa wa tatizo hilo kwamba nchi hii hadi sasa kuna mtu hana namba ya NIDA.

"Waziri wa Nchi, yupo hapa na ameshasikia hoja hii nzito kwasababu vijana wetu wanahitaji ajira, ikiwa kuna wilaya mahali ambapo ofisi za NIDA hazipo, hazina uwezo wa kutoa hizo namba katika kipindi hicho ambacho vijana wetu wanaomba kazi, hicho kigezo serikali mkiondoe kwasasa.

"Lakini kama ofisi za NIDA zipo kwenye wilaya zote na wanao uwezo wa kutoa hizo namba kabla ya muda kuisha wa kuomba hizi ajira, basi vijana wetu wakapate hizo namba kwa sababu tunataka kuajiri Watanzania sio watu ambao wanatoka sehemu nyingine halafu wapate hizo kazi serikalini," alisema Naibu Spika.

Katika mwongozo wake, Mbunge Kyombo, alisimama kwa kutumia kanuni ya 54 ya Bunge ambayo inasema baada ya muda wa maswali kuisha mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kama zilivyopangwa kwenye orodha ili lijadili jambo la dharura na muhimu kwa umma.


MARIPELANTO COMPANY LIMITED

N.I.C LIFE HOUSE, 6th Floor WING "C"
P.O Box 7839, Sokoine Drive/Ohio Street
+255 620559506 / +255 713341077
E-mail: maripelanto@outlook.com

TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **KENYA COMMERCIAL BANK TANZANIA LIMITED S. L. P. 804 DAR ES SALAAM** tunatoa notisi ya siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapa chini alipe madeni yake anayodaiwa muda mrefu na endapo atashindwa kulipa kwa muda uliotolewa dhamana itauzwa kwa mnada wa hadhara siku ya Jumamosi tarehe 02/06/2021 kuanzia saanne asubuhi huko Pugu Majohe mahali nyumba ilipo.

| S/No. | JINA LA MDAIWA | TAARIFA YA MALI | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1. | IMEX TECHNOLOGIES & GENERAL SUPPLIES | L. O. NO. 265898, PLOT NO. 2 BLOCK "D" 1390 SQM, CT No. 79231 INAYOMILIKIWA NA BWANA MAJALIWA THOBIAS KUZENZA | 02/06/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mteja anatakiwa kulipia asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% iliyobaki iwe imelipwa ndani ya siku kumi na nne (14).
2. Endapo mteja atashindwa kumalizia asilimia 75% ya salio lililobaki ndani ya siku kumi na nne(14), hatarudishiwa kiasi alicholipa mwanzo.
3. Mnunuzi atakabidhiwa mali aliyonunua baada ya kukamilisha malipo yote kwa asilimia mia moja (100%)
4. Kwa yeyote atakayeharibu mnada, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA MAWASILIANO WASILIANA NA MKURUGENZI MTENDAJI MARIPELANTO COMPANY LIMITED**
**Email: maripelanto@outlook.com**
**Phone: 0762610537**

Maripelanto Auctioneers & Court Brokers




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba na Balozi wa China, Wan Ke, wakibadilishana hati baada ya kutiliana saini mkataba wa kiasi cha Sh. bilioni 35.37 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WFM**

# China yaipa Tanzania mabilioni ya miradi

**Na Benny Mwaipaja**

SERIKALI ya China imeipatia Tanzania msaada wa Yuan za China milioni 100 sawa na Sh. bilioni 35.37 utakaotumika kutekeleza miradi itakayokubaliwa ama kuridhiwa na pande zote mbili.

Mkataba wa makubaliano ya msaada huo umesainiwa jana Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, kwa niaba ya Tanzania na Balozi wa China nchini, Wan Ke, kwa niaba ya China.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Tutuba alipendekeza utumike kupanua ujenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na kupandisha hadhi Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuwa Chuo Kikuu.

Pia alipendekeza kutekeleza mradi wa uhifadhi wa miamba katika eneo la Ngorongoro (Geopark), na miradi mingine itakayoafikiwa na serikali zote mbili.

Aidha, aliishukuru China kwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu inayoipatia Tanzania kuanzia mwaka 2010 na kutumika kujenga miundombinu ya reli, elimu, afya, Teknkolojia na Habari (TEHAMA), nishati, maji, sekta ya viwanda, kilimo, usalama, na misaada ya kitaalamu, iliyofikia dola za Marekani bilioni 1.8 sawa na Sh. trilioni 4.15.

"Nachukua fursa hii kukuhakikishia kwamba, Serikali ya Tanzania itachukua hatua zote muhimu kuhakikisha miradi itakayotekelezwa kwa fedha za msaada huu inakamilika kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa," aliongeza Tutuba.

Balozi wa China hapa nchini, Wan Ke alisema msaada huo ni matokeo ya ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, aliyoifanya mwezi Januari, mwaka huu na ni mwendelezo wa ushirikiano mwema kati ya nchi uliodumu kwa zaidi ya miaka 57 sasa.

"Tangu wakati huo China imeisaidia Tanzania kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwamo ujenzi wa reli ya TAZARA, uwanja wa michezo wa Benjamin Mkapa, ukumbi wa mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNCC), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam," alisema.

Aliitaja miradi mingine iliyofadhiliwa na China kuwa ni upanuzi wa Chuo cha Polisi Moshi mkoani Kilimanjaro, Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki jijini Dar es Salaam ambapo miradi hiyo yote imekabidhiwa serikalini.

"Tumewaleta madaktari wa kujitolea wapatao 25 ambao wamekuwa wakijihusisha na utoaji wa tiba ya moyo na kupambana na malaria maeneo mbalimbali nchini na hivi sasa pia China imefadhili ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi mkoani Kagera ambacho ukikamilika kitakuwa chuo kikubwa kuwahi kujengwa hapa nchini," alisema.

Pia alisema China imeipatia Tanzania msaada wa dola za Marekani milioni 1.3 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona kwa ajili ya kununulia barakoa, vitakasa mikono, vifaa tiba na dawa.

Kadhalika alisema nchi yake imetia saini kushiriki kwenye mpango wa kuahirisha ulipaji wa madeni (DSSI) ili kuruhusu serikali kuelekeza fedha hizo kwenye maeneo mengine katika kupambana na maradhi hayo.

# Askari JWTZ mbaroni madai kusafirisha wahamiaji

**Na LuLu George, TANGA**

JESHI la Polisi mkoani Tanga linawashikilia watu saba raia wa Bangladesh, kwa tuhuma za kuingia nchini bila kibali.

Katika tukio hilo, Polisi inamshikilia askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Koplo Rashid Mussa (38), ambaye alikuwa akiendesha gari lenye namba za usajili T 886 DVX, aina ya Toyota Alphard linalodaiwa kuwabeba wahamiaji hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi, Blasius Chatanda, alisema wahamiaji hao walikamatwa Mei 9, mwaka huu, majira ya saa 10.00 jioni katika Kijiji cha Negero, Tarafa ya Kimbe, Wilaya ya Kilindi.

Aliwataja wahamiaji hao ni Nahid Hassan(20), Abdullah Ahmmad(20), Mohamed Uddin (43), Abdul Hosen(43), Gaji Mahbub(44), Al Amin (21) na Nayeem Hassan(23).

Kwa mujibu wa Chatanda, wahamiaji hao walikuwa wakitokea Kabuku, Wilaya ya Handeni kuelekea mkoani Morogoro.

Kuhusu askari huyo wa JWTZ, Kamanda Chatanda alisema: "Bado uchunguzi unaendelea kwanza kujua kama huyu aliyejitambulisha ni askari wa JWTZ, kama ni askari kweli.

"Lakini nani mwingine anashirikiana naye, na kimsingi tunafuatilia kujua kwamba hawa Wabangladesh wamekuja kwa dhamira gani. Je, ni wahamiaji haramu wa kawaida au wanaenda kungana na wahalifu wa Kaskazini mwa Msumbiji? Haya ni mambo ambayo bado tunayachunguza."

Alisema bado wanashangazwa kuwaona raia wa Bangladesh wakipita Tanzania, tofauti na wahamiaji ambao wamezoeleka kutoka nchi za Somalia na Ethiopia.

Hata hivyo, Kamanda Chatanda alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea na watuhumiwa watachukuliwa hatua za kisheria baada ya upelelezi kukamilika.

**HABARI KITAIFA**

# Mahindi ya Tanzania yaanza kuingia Kenya

**Na Waandishi Wetu**

WIKI moja baada ya Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, kuruhusu mahindi ya Tanzania yaliyokuwa yamezuiliwa mipakani kuingia nchini humo, wafanyabiashara wameanza kupitisha shehena ya mahindi bila kikwazo kupitia mipaka ya Holili, Namanga na Tarakea.

Wakati mipaka hiyo ikifunguka, jana Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Peter Mathuki, alitembelea Kituo cha Forodha cha Namanga kilichopo Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

Mathuki alikwenda kufuatilia utelekezaji wa agizo la wakuu wa nchi za Tanzania na Kenya la kutaka kuondolewa vikwazo vya kibiashara katika mipaka inayotenganisha nchi hizo.

Akiwa Namanga, Mathuki alitembelea idara zake na kuzungumza na watendaji ambao walimweleza matatizo mbalimbali yanayowakabili likiwamo la tofauti ya utekelezaji wa majukumu yao licha ya kuwa katika kituo cha pamoja cha forodha.

Alielezwa tofauti hizo kuwa ni viwango vya ubora wa bidhaa, vitendea kazi na mifumo ya utoaji wa huduma katika kituo hicho.

Akizungumza baada ya kuwasikiliza maofisa wa forodha wa pande zote mbili, Katibu Mkuu huyo wa EAC, alisema ziara yake imekuwa na mafanikio makubwa, kwa kuwa amebaini matatizo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kituo cha Pamoja cha Forodha cha Mpaka wa Horohoro, mpaka kufikia jana, hakuna mfanyabiashara ambaye amepita na shehena ya mahindi au lori lililopita katika mpaka huo.

Miongoni mwa mambo aliyodai yanahitaji kufanyiwa kazi ni pamoja na kujenga ushirikiano miongoni na watendaji wa kituo hicho cha forodha na kuhakikisha wanashirikiana pamoja na kwa dhati katika utendaji wao wa kazi.

Awali, madereva wa malori, walimweleza Mathuki tatizo la tofauti ya viwango vya tozo za kupima virusi vya corona na muda wa kupata majibu.

Wakizungumzia suala la mahindi yaliyokuwa yamekwama, watendaji wa Mamlaka za Mapato za Tanzania na Kenya, akiwamo Paul Kamukuli wa TRA-Tanzania na Joseph Monywanywa wa KRA-Kenya, walisema hivi sasa mahindi hayo yameanza kupita bila kikwazo.

Alipoulizwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido ulipo mpaka wa Namanga, Dk. Juma Mhina, alisema kwa sasa mahindi yanayotoka mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Kaskazini kwenda Kenya, yameanza kupita kwa wingi katika mpaka huo.

●**Imeandikwa na Asraji Mvungi, Zanura Mollel (Arusha), Lulu George (Tanga) na Mary Mosha (Kilimanjaro) na Lulu George (Tanga)**

# RAS ataka uhakiki mizani za mazao

**Na Mwandishi Wetu, LINDI**

VIONGOZI wa vyama vya msingi vya ushirika mkoani Lindi, wametakiwa kuhakikisha mizani zote zitakazotumiwa katika ununuzi wa mazao zihakikiwe na kuwekewa alama maalumu za Wakala wa Vipimo (WMA).

Wito huo ulitolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Lindi, Rehema Madengea, wakati wa mafunzo yaliyotolewa na WMA, akisema elimu ya vipimo ni mwafaka mkoani humo kwani msimu wa ununuzi wa mazao unakaribia kuanza.

Rehema aliwaeleza wafanyabiashara na viongozi wa vyama vya msingi kuwa wizi wa aina yeyote ni kosa la jinai, hivyo hata kuibia wananchi na wakulima kwa kuchezea vipimo ni kosa la jinai, na yeyote atakaye kamatwa kujihusisha na vitendo vya uchezeaji wa vipimo atakamatwa na kuchukuliwa hatua stahiki.

"Nawasihi sana wanunuzi wa mazao kuacha kutumia vipimo batili kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwanyonya wakulima ndio maana wafanyabiashara wanaendelea kwa kasi huku wakulima wanabaki katika hali duni ya kiuchumi itoshe kusema vitendo hivyo havikubaliki imefika wakati mkulima inabidi apate tija kunufaika na kile anachokizalisha kwa kuuza mazao kwa kutumia vipimo sahihi (mzani)," Katibu Tawala Mkoa wa Lindi alieleza.

# M'biashara nyama asakwa tuhuma kuchinja ng'ombe, mbuzi wa wizi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani, linamsaka mfanyabiashara wa nyama (jina limehifadhiwa) kwa tunuma za kuchinja mifugo ya wizi na kuuza kwenye mabucha yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jeshi hilo lilipokea taarifa za kupotea kwa ng'ombe 25 na mbuzi 31, mali ya Rajabu Maulid (69), yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 na kuanza operesheni.

Alisema mifugo hiyo iliibiwa na mchungaji aliyefahamika kwa jina moja la George, ambaye alimuuzia mfanyabiashara huyo anayesakwa na kuchinja baadhi ya ng'ombe katika mazingira yasiyo salama, kuingiza nyama katika mabucha yake na kuwauzia walaji.

Kamanda alisema msako wa Polisi umenasa mabucha saba katika maeneo ya Picha ya Ndege, Kwamatiasi, Loliondo, Kilivya Kwakomba, bucha zote zinadaiwa kumilikiwa na mfanyabiashara huyo.

Alisema vitu vilivyokamatwa katika msako huo ni kilo 235 za nyama iliyokamatwa na kuteketezwa na wataalamu wa Idara ya Mifugo, ng'ombe wanne mali ya Rajabu Maulid, ambao aliwatambua.

Vitu vingine vilivyokamatwa ni ngozi za ng'ombe nane ambao walichinjwa, mbuzi 24, mali ya Rajabu.

Katika operesheni hiyo walikamatwa watuhumiwa watano Zacharia Chiteme (25), Samwel Paschal (18), Antony Ngaliya (25), Abdallah Athumani (23) na Aidan Simon (43), wote wafanyakazi katika mabucha ya mtuhumiwa. Kamanda ametoa wito kwa mtuhumiwa kujisalimisha katika kituo chochote cha polisi na kuwasihi wananchi kutonunua nyama ambayo haikuthibitishwa na wataalamu wa Idara ya Mifugo.

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **JOSINACOMPANY LIMITED AND AUCTIONEER, MUGABO AUCTION MART AND COMPANY LIMITED na MASE INTERNATIONAL LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD**, Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| NOTISI KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | | |
|---|---|---|---|
| | MUGABO AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | SISTER Y. NYAKUBA | GARI AINA YA NISSAN WINGROAD YENYE NAMBA YA USAJILI T515 CPF NA KIWANJA NA. 521 KITALU T | MWISENGE-MUSOMA |
| 2 | NUNIBI V. KISHANTA | NYUMBA NA KIWANJA | KOMUGE RORYA NA NYAKATO |
| 3 | NYAMHANGA MASWI | NYUMBA | BWERI -MUSOMA |
| 4 | FRANCIS DAVIS MCHACKY | GARI AINA YA FORD ECO SPORT YENYE NAMBA YA USAJILI T884DEM | MUSOMA MJINI |
| 5 | FRED D. MASANO | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 771 KITALU T | MUSOMA MJINI |
| 6 | SWAHIBU M. EBUTURA | NYUMBA | BARUTI -MUSOMA |
| 7 | RAMADHAN IBRAHIM JUMA | NYUMBA | MGANGO- MUSOMA |
| 8 | MAPAMBANO FESTUS FUPI | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA.528, KITALU 'U' | MUTEX - MUSOMA |
| 9 | SAID ABUU KIRIA | KIWANJA | NYABANGE- BUTIAMA |
| 10 | MARWA JAMES ROBI | KIWANJA | MANYAMA NYAMA BUNDA MJINI |
| 11 | JAMIL SAID SEIF | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 242 KITALU " F' | BUNDA MJINI |
| 12 | CONSOLATA LADISLAUS MTAKI | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 263 KITALU Q | CHIRINGE BUNDA MJINI |
| 13 | STIVINE K. GAREMBANA | NYUMBA | MIEMBENI, MANYAMA NYAMA- BUNDA |
| 14 | SOPHIA O. DANIEL | KIWANJA | MIEMBENI, MANYAMA NYAMA- BUNDA |
| 15 | JOHN M. ANDREW | NYUMBA | NYABANGE-BUTIAMA |

| JOSINA COMPANY LIMITED AND AUCTIONEER | | | |
|---|---|---|---|
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 9 | AZAM BAITWA | NYUMBA | IGABILO |
| 10 | STIVEN NYOISA | KIWANJA | MAGOTI- KIBETA |
| 11 | PIUS F. BAJWALA | NYUMBA | KEMONDO |
| 12 | HEKIMA N. ELIYA | KIWANJA | BULUMBA BUGABO |
| 13 | BENSON B. BISONGOE | KIWANJA NA NYUMBA | KEMONDO |
| 14 | DESDERY E. MACHUME | NYUMBA | KILIMAHEWA-BUKOBA |
| 15 | FATAKI ABDALLAH | KIWANJA NA NYUMBA | KASHAI PEPSI |
| 16 | SHAKIRU O. RUGONZIBWA | BOMA LA NYUMBA | IZIGO |
| 17 | ADOLPH S. RUHIMBIZA | KIWANJA | KYAKAILABWA- NYANGA |
| 18 | NEEMA S. NURU | KIWANJA NA NYUMBA | RWAMISHENYE-BUKOBA MJINI |
| 19 | MUSWADIKU M. AMADA | KIWANJA | NYAKANYASI |
| 20 | SHUBIRA T. KISHENYE | KIWANJA | KARAGWE |
| 21 | KHALID GALIATANO | NYUMBA | MIGERA-BUKOBA MJINI |

| | MASE INTERNATIONAL | | |
|---|---|---|---|
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 22 | JOSEPH CHACHA JOHN | NYUMBA .527, KITALU ' BUJINGWA | BUSWELU-BUJINGWA (TAREHE YA MARUDIO YA MNADA 19/5/2021 NA KUENDELEA |
| 23 | GEORGE PETER MISSOKE | NYUMBA | NYABISAREI-MUSOMA |
| 24 | FULGENCE F.GABLIEL | NYUMBA | MLIMANI-MUSOMA |

### MASHARTI YA MNADA

1. Ukaguzi wa dhamana husika unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo, mahali ilipo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) kutoka tarehe ya mnada, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

### KWA MAWASILIANO ZAIDI

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mugabo Auction Mart and Company Limited**
**S.L.P 766 Musoma**
**Simu; 0755555295/ 0673672848**

**Na Mkurugenzi Mtendaji**
**Josina Company Limited And Auctioneer**
**0713203040**

**Na Mkurugenzi Mtendaji**
**S.L.P**
**Simu NAMBA**
**0784717164**

**Na**
**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Mobile: 0768790399, 0754774949**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusiwape watu chanjo ya corona kwa kukurupuka

**TUNALIPONGEZA** Bunge kwa kukumbusha jambo la msingi la afya ya Watanzania kuhusu chanjo ya corona, ambayo hadi sasa haijawa na jawabu la kuridhisha na kujitosheleza kwani ukweli kuhusu maradhi hayo yanayoshambulia njia na mfumo wa hewa haujafahamika kikamilifu.

Serikali imetangaza kuunda kamati ya kuishauri kuhusu masuala ya corona na ikiwamo pia chanjo, lakini ukweli ni kwamba tatizo la maradhi hayo ni kubwa kutokana na ugeni, njia za kusambaa, virusi kujibadilisha kila wakati na taathira kwa waathirika.

Yote hayo yanahitaji utaalamu, ujuzi na utafiti zaidi licha ya kwamba mataifa mengi yaliyoendelea yameanza kutoa chanjo kwa watu wao huku baadhi ya nchi za Afrika zikitoa pia.

Lakini, kama Bunge linavyoshauri hakuna sababu ya papara kwani hata mataifa yaliyoendelea mfano, Canada yako makini kupindukia.

Mathalani, Wizara ya Afya nchini humo imeidhinisha chanjo ya Moderna kwa watoto walio na miaka 18 tu, wakati Pfizer-BioNTech inatolewa kwa watoto wenye miaka 12 kwa sababu imethibitisha kuwa inaweza kuwakinga watoto wenye umri huo, lakini si wadogo zaidi.

Taifa hili pia limeidhinisha chanjo ya The Jonson and Jonson-Janssen au Ad26.COV2 inayotolewa kwa yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka 18.

Tukirejea kwa upande wa Afrika, Kenya majirani zetu, Afrika Kusini na Nigeria zimetoa chanjo.

Lakini cha kusikitisha zaidi, hakuna utafiti uliofanywa vya kutosha hadi kufikia maamuzi ya kuanza kuwapa chanjo wafanyakazi wa afya.

Hili ni jambo lililohitaji kufikiria na kuchunguza zaidi kwa vile ikitokea chanjo hiyo ikiwa na athari inamaanisha umeangaza jeshi la matatibu na itabidi kuanza upya.

Hili ni suala la msingi, kuacha kutoa chanjo kwa kukurupuka. Kenya imepokea chanjo ya Astra Zeneca na kampeni zimeanza na wafanyakazi wa sekta ya afya kwanza.

Kadhalika Nigeria nayo inatoa chanjo ya AstraZeneca ikiwapa pia watumishi wa sekta ya afya kwanza.

Afrika ya Kusini pia wanatoa chanjo ya Johnson & Johnson Jenssen kwa wafanyakazi wa afya ni wa kwanza kuchanjwa ili kuongeza imani ni Rais wa taifa hilo, Cyrill Ramaphosa na viongozi wengine wa sekta hiyo.

Ni wazi kuwa kutoa chanjo kienyeji kama kuamua taifa zima lichanjwe Astra Zaneca au Jenssen huenda si sahihi ndiyo maana Canada wamekwenda mbali zaidi kujua na kupanga umri wa wahusika. Umakini unahitajika kwa vile hadi sasa haifahamiki iwapo ukipewa chanjo una uwezo wa kuambukiza wengine au la.

Na pengine haifahamiki kama chanjo ni salama kutokana na kubadilika kwa virusi hatua inayoitwa kitaalamu 'mutation'.

Swali linakuja iwapo chanjo ina madhara na inaweza hata kutishia maisha itakuwaje kama tumewachanja madaktari, wauguzi na wafanyakazi wote wa sekta ya afya?

Ni wazi kuwa kuna haja ya kufikiria sana na kuchunguza na kufuatilia hatua kwa hatua kwa makini kabla ya kuchanja watu.


Inavyoelekea kuna haja pia ya kufahamu aina ya kirusi cha corona kinachosumbua taifa, kwa mfano Afrika Kusini ilianza na Astra Zeneca, lakini ikaonekana kuwa kuna jamii mpya ya kirusi na kuanza kutoa chanjo ya Jessen.

Kama Bunge lilivyoshauri nasi tunaunga mkono kuwa si lazima kutoa chanjo kwa Watanzania kama wataalamu hawafahamu hatima ya nini tunachokifanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wauguzi hawa mfano wa kuigwa kupunguza mimba za wanafunzi

**JANA** ilikuwa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani, ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Manyara, yakiwa na kaulimbiu: "Wauguzi sauti inayoongoza, Dira ya huduma ya afya".

Maadhimisho hayo hufanyika Mei 12 kila mwaka, hapa nchini, zilifanyika shughuli mbalimbali ikiwamo za kuelimisha wanafunzi mada mbalimbali zinahusu utunzaji wa afya.

Miongoni mwa wanafunzi waliopata elimu hiyo, ni wa Shule ya Sekondarii Malamba-Mawili, jijini Dar es Salaam, ambao waliofundishwa na wauguzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wa Upanga na Mloganzila.

Wauguzi hao walikuwa katika shule hiyo juzi, wakifundisha fani ya uuguzi, athari za matumizi ya dawa za kulevya, jinsi ya kujikinga na mimba za utotoni na kufahamu njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza.

Moja ya magonjwa hayo ya kuambukiza ni UKIMWI. Lakini wanafunzi hao, walifundishwa kuhusu kutambua mabadiliko ya mwili yanayotokana na ukuaji na madhara ya mimba za utotoni.

Walihamasisha pia wanafunzi kujiunga na fani ya uuguzi pamoja na jinsi ya kuboresha afya ya jamii, afya ya akili, afya ya uzazi, usafi na namna ya kutoa huduma ya kwanza shuleni.

Binafsi ninaamini kuwa hatua zilizofanywa na hospitali hiyo zinafaa kuigwa na kuzindeleza katika shule mbalimbali nchini, ili kusaidia kupunguza tatizo la mimba shuleni ambalo linaendelea kuwambuka wanafunzi.

Mkuu wa Wilaya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, alisema katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Januari hadi Julai mwaka 2019 jumla ya wanafunzi 119 walikatisha masomo kwa kukumbwa na tatizo hilo.

Hiyo ni wilaya moja tu na kwa kipindi kifupi cha miezi tisa, hali kama hiyo inawezekana ipo katika wilaya zote nchini, na kama ndivyo, tatizo hilo ni kubwa ambalo linatakiwa kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mimba hizo katika Wilaya ya Tunduru, zilimfanya mkuu wa wilaya hiyo kuwaomba wazee washirikiane kikamilifu na serikali kwa ajili ya kutokomeza tatizo hilo.

Mtatiro anaeleza kuwa, sababu kubwa ya kuwapo kwa mimba wilayani mwake ni kukosa uangalizi wa wazazi, kwa kuwa jamii inawaacha watoto kujihudumia wenyewe.

Lakini pia anasema wazazi kutojali wanafunzi wanapopata mimba na mila na desturi hasa unyago, vinachangia kuwapo kwa ongezeko kubwa la tatizo hilo ambalo hukatisha ndoto za wanafunzi.

Kwa hali hiyo, ni wazi kwamba, elimu kama hiyo iliyotolewa na wauguzi inaweza kuwa na manufaa makubwa katika vita dhidi ya mimba shuleni au mimba za utotoni ambazo ni kero.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wake, ipo haja pia kuwekwa mkakati wa kutembelea shule zote nchini mara kwa mara na kutoa elimu kama hiyo.

Wauguzi hao wametoa elimu hiyo wakati huu wa maadhimisho ya siku yao, baada ya hapo inawezekana wakasubiri hadi maadhimisho ya mwaka ujao, hali ambayo inaweza isizae matunda kwa kutokuwa endelevu.

Kwa maana hiyo, ingependeza iwapo wadau wote wataunga mkono kile ambacho wauguzi hao wamekianzisha na kukiendeleza kwa kuzunguka katika shule zote nchini mara kwa mara na kuwaelimisha wanafunzi.

Kimingi, wauguzi waliokwenda kutoa elimu ya afya katika Sekondari ya Malamba-Mawili, wamefanya jambo jema ambalo ni mfano wa kuigwa, ila na wasiishie hapo, uwe ni utaratibu endelevu katika shule mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa mara nyingi huwa kuna taarifa za kuwapo kwa mimba shuleni, lakini suala la usalama wa afya zao halijulikani, hali ambayo ni wazi kwamba ipo haja ya kuwaelimisha ili waepuke pia madhara ya kiafya.

HABARI KITAIFA

# Wakaguzi watakiwa kudhibiti wizi wa dawa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, amewataka wakaguzi wa dawa na vifaa tiba mkoani humo kudhibiti wizi wa dawa za serikali ambazo hupelekwa nchi za jirani.

Ndungile alibainisha hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya wakaguzi wa dawa na vifaa tiba mkoani humo yaliyoshirikisha wafamansia, waratibu wa maabara na mifugo yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA). Alisema Mkoa wa Shinyanga kwa upande wa Kahama unapakana na nchi jirani za Burundi, Rwanda na kufanya iwe rahisi dawa za serikali kupelekwa huko. “Naomba sana wakaguzi wa dawa na vifaa tiba, mzingatie maadili ya kazi yenu na kudhibiti wizi wa dawa za serikali na uingizwaji holela wa dawa na vifaa tiba ambavyo havijasajiliwa kuingizwa hapa nchini, ili kulinda afya za wananchi wetu,” alisema Ndungile.

Aliwataka wakaguzi hao kudhibiti maduka ya dawa bubu na maabara kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa ili kumaliza tatizo la uuzwaji holela wa dawa ambazo ni bandia, duni, zilizokuwa na usajili, pamoja na zile zilizomaliza muda wake.

Kwa upande wake Meneja wa TMDA, Kanda ya Ziwa Magharibi, Dk. Edga Mahundi, aliwaagiza wakaguzi hao wakikamata watuhumiwa wasiombe rushwa badala yake wawachukulie hatua kali za kisheria.

Alisema uingizwaji wa dawa holela hapa nchini na vifaa tiba ni kuitia hasara serikali pamoja kudhorotesha uchumi wa nchi.



Watuhumiwa wa kesi ya kupatikana dawa za kulevya aina ya Heroin kilo 20.24, wakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa mashtaka. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yasisitiza msimamo kuhusu ugonjwa wa corona

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

SERIKALI imesema haipishani na dunia kuhusu suala la corona, bali inataka kujiridhisha na tafiti za kisayansi kuhusiana na chanjo kabla ya kufanya maamuzi kwa ajili ya Watanzania. Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Molel, wakati akijibu hoja zilizoibuliwa na wabunge wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2021/22. Alisema serikali kwa namna yoyote ile haipingani na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), na Tanzania haijioni ni kisiwa, na kwamba inakubailiana na mambo yote ya kisayansi na afya yanayotokea duniani.

“Ubishani haupo kati ya serikali au wizara na mtu yeyote, ubishani upo kati ya wanasayansi kuhusu usalama wa kitu tunachoenda kufanya. Ubishani siyo kutofautiana tunaulizana kisayansi unaposema hiki kinaingia kwenye celi hakikuzi DNA lazima tuelewane,” alisema.

Alitolea mfano suala la umbile la mimea ambayo mapapai yalifanyiwa maboresho kisayansi mwaka wa kwanza yakazaa mengi na makubwa na baada ya miaka miwili yalizaa mapapai yasiyo na mbegu.

“Tunajiuliza maswali mengi kwamba kwa binadamu usalama uko wapi, lakini tukubaliane kuwa dunia inakoelekea chanjo nyingi zitatengenezwa kutokana na RNA (kiini) na maumbile (genetic),” alifafanua na kuongeza: “Anachokifanya Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan ni kwamba anataka kuhakikisha hata kama tunakubaliana na duniani tuhakikishe tuko salama kabisa.” Alisema kamati ya wataalamu ambayo inajumuisha maprofesa waliobobea iliyoundwa na Rais inafanya umakini juu ya nini kinaingia na kufanyika kwa ajili ya wananchi.

Dk. Molel alifafanua kuhusu chanjo zitokanazo na RNA zinaingia kwenye seli lakini hazigusi DNA, na kwamba wataalamu wanaangalia ukweli wa suala hilo kabla nchi haijasema lolote. Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, chanjo ambazo ni DNA watafiti wanatumia virusi kutoka kwa Sokwe Mtu na kuchanganya na ‘Adenovirus type 5’ ambayo katikati kuna kirusi cha corona na pembeni kuna ‘type 5’ ambaye anaingia kwenye nyuklia na kutengeneza protini.

NHC
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TANGAZO KWA WAPANGAJI MKOA WA DAR ES SALAAM

1. Tunapenda kuwafahamisha wapangaji wetu waliopo Mkoa wa Dar es Salaam kuwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limeanzisha Mkoa mpya wa Dar es Salaam Metropolitan. Uamuzi huu wa Shirika unalenga kusogeza huduma zetu za upangaji kwa wateja wetu.
2. Mkoa huu wa Dar es Salaam Metropolitan umetokana na kumegwa maeneo yaliyokuwa katika Mikoa yetu ya Upanga na Ilala.
3. Maeneo yanayounda Mkoa huu mpya wa NHC yanahusisha majengo yote yaliyopo katikati ya mitaa ya Azikiwe upande wa Mashariki, Mtaa wa Mosque upande wa Magharibi, Barabara ya Sokoine upande wa Kusini na Bibi Titi Mohamed upande wa Kaskazini.
4. Tunawaomba wateja wetu wanaopanga na kuishi katika maeneo hayo, wafahamu kwamba kuanzia tarehe 1 Juni 2021 watakuwa wanahudumiwa na Mkoa huo mpya. Ofisi za Mkoa huu zipo katika jengo la Diplomat kiwanja Na. 26 kwenye makutano ya Barabara ya Mkwepu na Kaluta ghorofa ya sita.
5. Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linaahidi kuwa litaendelea kuwapa wapangaji wa Mkoa huu mpya huduma bora za upangaji kama ilivyokuwa katika mikoa yao ya awali.

**LIMETOLEWA NA:**
**KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA | SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000
BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com

# Wakaguzi wa hesabu watakiwa kuwa wajuzi

**Na Beatrice Moses**

OFISI ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) imesisitiza umuhimu wa wakaguzi wa hesabu kuwa na ujuzi sahihi unaoweza kuwasaidia kuzikabili changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Novati Mfalamago, aliyemwakilisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika uzinduzi wa mafunzo ya stashahada ya Mfumo wa Kimataifa wa Kutoa Taarifa na Uandaaji wa Hesabu (IFRS) kwa wakaguzi 20 kutoka ofisi ya NAOT iliyofanyika Dar es Salaam.

"Mafunzo haya yatakayochukua wiki tano yameandaliwa maalum kwa ajili ya wakaguzi wa hesabu kutoka ofisi ya NAOT ili kuwajengea uelewa mpana zaidi kuhusiana na IFRS," alisema.

Aliwataka washiriki kujituma wakati wote wa mafunzo ili kupata elimu kubwa itakayotolewa na wawezeshaji wa mafunzo hayo.

Mfalamagoha alisema zaidi ya kutakiwa kufaulu vizuri mitihani yao, pia wanafunzi hao wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanapata uelewa mkubwa wa mfumo wa IFRS na kuutumia katika majukumu yao ya kila siku.

Mkuu wa Bodi ya Wahasibu ya Kimataifa (ACCA) nchini, Jenard Lazaro, alisema elimu itakayopatikana katika mafunzo haya itawajengea washiriki uelewa mkubwa sana wa mfumo wa IFRS na namna ya kuitumia katika majukumu yao ya kihasibu.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Godfrey Temba, alisema mafunzo haya ya stashahada yatawawezesha washiriki kutoka ofisi ya NAOT kuweza kupata utaalamu wa kimaarifa na kivitendo kupitia mafunzo haya ya stashahada ya IFRS.

Naye Mkurugenzi wa ACCA Africa, Jamil Ampomah, alisema mafunzo ya stashahada ya IFRS yana lengo la kutoa suluhisho la haraka litakalowasaidia wataalamu wa fedha kupata elimu na utaalamu wa kufanya kazi katika mazingira mbalimbali.




Mkuu wa Bodi ya Wahasibu ya Kimataifa (ACCA) Tanzania, Jenard Lazaro, akiongea katika uzinduzi wa mafunzo ya stashahada ya Mfumo wa Kimataifa wa Kutoa Taarifa na Uandaaji wa Hesabu (IFRS) kwa wakaguzi 20 kutoka ofisi ya NAOT yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara Soko Mkuti watangaza mgomo kulipa ushuru

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAFANYABIASHARA zaidi ya 600 wa Soko Kuu la Mkuti wilayani Masasi, mkoani Mtwara, wametangaza mgomo wa kutolipa ushuru wa mabanda wanayofanyia biashara kwa Halmashauri ya Mji Masasi kutokana na kutokuwa na imani na wakusanyaji ushuru.

Wafanyabiashara hao wamedai kubambikiziwa madeni hewa pamoja na kuwatoza ushuru kiholela na kutopatiwa risiti pale wanapolipa ushuru wa mabanda yao.

Waliyasema hayo katika mkutano wa dharura wa umoja wa wafanyabiashara wa soko hilo, uliolenga kukutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, Gimbana Ntavyo, ambaye hata hivyo, hakuwapo katika mkutano huo.

Wakizungumza katika mkutano huo, wafanyabiashara hao walisema kuwa azimio lao hilo lililoanza Mei 5 limefikiwa kutokana na mkurugenzi huyo kushindwa kufika katika mkutano huo kwa ajili ya kuwasilikiza wafanyabiashara hao kuhusu kero zao za kuandikiwa madeni hewa na kulipishwa ushuru bila ya kupewa risiti na wakusanyaji wa ushuru wa halmashauri hiyo.

Akizungumza na wafanyabiashara hao, Mwenyekiti wa soko hilo, Abdalah Mtandama, alisema hawakubaliani na taarifa iliyotolewa na halmashauri hiyo ya kuwapo wafanyabiashara wanaodaiwa ushuru wa mabanda.

Mtandama alisema taarifa hiyo haipo sahihi kwa sababu wafanyabiashara ambao wameorodheshwa kwenye taarifa hiyo wapo ambao hawadaiwi na kila mwaka wanalipa ushuru huo.

Alisema baada ya kujitokeza mkanganyiko huo walimwomba mkurugenzi wa halmashauri hiyo kwenda kukutana na wafanyabiashara hao na kumweleza uhalisia wao kutokuwa na madeni.

Hata hivyo, alisema mkurugenzi hakufika na hakutoa taarifa yoyote hali iliyowalazimu kutangaza mgomo.

Zaurati Khamisi, mfanyabiashara katika soko hilo, alisema kuwa ameshangazwa kuona ameandikiwa madai ya zaidi ya Sh. 300,000 wakati deni lake halisi ni Sh. 30,000 ambalo ni la miezi mitatu na kwamba ushuru wa fedha za miezi iliyopita aliyolipa hajapewa risiti.

Alisema kutokana na kero hizo wafanyabiashara wameona ni bora wasitishe kulipa ushuru wa mabanda hadi pale mkurugenzi atakapokutana nao.

Gistus Joseph, mfanyabiashara wa soko hilo alisema anamiliki vibanda viwili na analipa ushuru kila mwaka, lakini wakusanyaji hawatoi risiti.

Alisema ameshangazwa baada ya kuletewa taarifa ya kuwa ana deni la Sh. 460,000.

Mfanyabiashara mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Abdalah Mkeng'endo, alisema wakusanyaji ushuru wa halmashauri hawatumii utaratibu wa serikali wa ukusanyaji wa ushuru ambao mtozwa ushuru ni lazima apatiwe risiti.

Naye Hamisi Selemani alisema wamekosa imani na wakusanyaji ushuru wa halmashauri kwa madai kuwa wana tabia ya kuwaandikia madeni hewa wafanyabiashara.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntavyo, alikiri kupokea barua ya wafanyabiashara hao inayomtaka kuhudhuria mkutano huo. Alisema wafanyabiashara kulipa ushuru ni jambo la kisheria na kwamba wanapaswa kuendelea kama sheria inavyotaka.

# NHIF yaokoa mil. 600/- malipo hewa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mkoa wa Kagera, umeokoa Sh. milioni 600 ambazo zilighushiwa kama malipo hewa na watoa huduma kwa wanachama wa mfuko huo. Watoa huduma hao walipeleka madai ya Sh. bilioni 5.8 walizokuwa wanadai NHIF, lakini baada ya Mfuko kuhakiki madai hayo uligundua kiasi walichokuwa wanadai ni Sh. bilioni 5.2. Meneja wa NHIF mkoani humo, Mathias Sweya, alisema baada ya kupokea taarifa ya madai ya Sh. bilioni 5.8 kwa vituo 330 vinavyotoa huduma walibaini udanganyifu.

Alisema baada ya uhakiki baadhi ya vituo vilibainika kuongeza vituo ambavyo mwanachama hawajapatiwa huduma hiyo.

"Hatukuweza kulipa madai hayo kwa sababu wapo watoa huduma ambao ni wadanganyifu wa kuomba madai ya malipo yasiyo halali kwa kuongeza vituo ili kutaka kujipatia pesa ndio maana huwa hatulipi kabla ya kufanya ufuatiliaji wa hatua kwa hatua kwenye vituo vyetu," alisema.

Alisema maeneo ambayo wanachama wao wanapata huduma ni pamoja na hospitali, vituo vya afya, zahanati na maduka ya dawa yaliyokidhi vigezo.

Alisema kwa miezi 10 kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021, mfuko huo ulifanya malipo ya Sh. bilioni 1.9, kwa vituo vya dini, serikalini Sh. bilioni 1.6, binafsi Sh. bilioni 1.2 na maduka ya dawa Sh. milioni 760.

## Wanafunzi wapewa elimu bidhaa zilizothibitishwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WANAFUNZI wa Shule za Msingi na Sekondari wamepewa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothibitishwa na kusajiliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Elimu hiyo iliyoanza kutolewa tangu Mei 4, mwaka huu, imetolewa kwenye shule, minada, magulio katika maeneo mbalimbali ya Wilaya za Kilosa, mkoani Morogoro na Mkinga, mkoani Tanga. Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, pia wamewapa namba ya mawasiliano kwa ajili ya kupiga bure kuwasiliana na shirika hilo ikitokea wakapata matatizo au changamoto kwenye bidhaa. Alisema wamefikisha elimu hiyo kwa wanafunzi kwa kutambua kwamba wataenda kuwa mabalozi wazuri kwa wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothibitishwa na TBS.

Kwa upande wa maeneo yenye mikusanyiko ya watu, Mtemvu alisema elimu hiyo imetolewa Mkinga katika Stendi ya Hororo na gulio la Duga, huku kwa upande wa Kilosa elimu hiyo ikitolewa Uhindini, Sabasaba na Kimamba.

Kuhusu mwitikio wa wananchi katika maeneo hayo yenye mikusanyiko ya watu, Mtemvu alisema wengi wamefurahishwa na elimu hiyo na wameomba iwe endelevu.

"Wananchi wameshukuru shirika kwa kuona umuhimu wa kuwapatia taarifa hizo kuhusu viwango kwa sababu wamekuwa wakipata changamoto kubwa, lakini walikuwa hawajui wafanyaje," alisema.

Alisema kwa sasa wenyewe wameahidi kuingia kwenye vita ya bidhaa hafifu kwa sababu wana uwezo wa kuwasiliana na TBS.

Alisema miongoni mwa mambo waliyoelimishwa wananchi hao kupitia kampeni hiyo ni pamoja na majukumu ya TBS, umuhimu wa kuangalia tarehe ya mwisho ya matumizi ya bidhaa wanazotaka kununua.

Alisema eneo lingine ambalo wananchi hao walielimishwa ni umuhimu wa wao kununua bidhaa zilizothibitishwa na kusajiliwa na TBS.

Mtemvu alitaja baadhi ya faida za kununua bidhaa zilizothibitishwa na shirika hilo kuwa ni pamoja na kulinda afya zao na thamani za fedha zao.

# RC aagiza ofisa ardhi kukamatwa na kuhojiwa

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amemwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Nzega kumkamata Ofisa Ardhi, Elisha Luponije, kwa ajili ya mahojiano dhidi ya tuhuma zinazomkabili za kuchukua fedha kwa baadhi ya wakazi Bukene kinyume cha maelekezo ya serikali.

Alisema mtumishi huyo anatuhumiwa kwenda Kata ya Bukene kwa lengo la kuhakiki nyumba ambazo zinatakiwa kulipa pango la ardhi, lakini yeye alichukua fedha kwa madai ya kulipwa gharama za ofisi, vibali vya ujenzi na gharama za kubadilisha umiliki wa nyumba kwa watu waliouziana.

Dk. Sengati alitoa kauli hiyo jana baada ya wakazi wawili wa Kata ya Bukene, kumtuhumu ofisa huyo kwa kuchukua fedha zao zaidi ya Sh. 900,000 bila ya kuwapa stakabadhi ya kuonyesha kama malipo hayo ni halali.

Alisema ofisa huyo alidiriki hata kuwadanganya wananchi hao kuwa sehemu ya fedha hizo ni kwa ajili ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kama gharama za kubadilisha umiliki wa nyumba na hata hivyo hakizipeleka sehemu husika.

Mkazi wa kwanza wa Bukene, Fredy Richard, alisema mtuhumiwa alifika nyumbani kwake na kumtaka alipe Sh. 390,000 ikiwa ni gharama za kibali cha ujenzi na ubadilishaji wa umiliki wa nyumba baada ya kuinunua kutoka kwa mtu mwingine na gharama za kibali cha ujenzi.

Alisema pamoja na kutekeleza agizo hilo imepita miezi zaidi ya sita hayajawahi kupata nyaraka yoyote inayoonyesha kulipa fedha hizo.

Naye Ibede Luhaga, alisema yeye alidaiwa Sh. 560,000 kama gharama ya ofisi, TRA, kibali cha ujenzi na kubadili hati ya umiliki kutoka kwa aliyemuuzia nyumba kwenda kwake.

Alisema pamoja na kulipa fedha, lakini kila alipofuatilia apate hati ya umiliki wa nyumba aliishia kutupiwa matusi na ofisa huyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Seleman Sikieti, alikiri kumfahamu mtumishi huyo na kuwa yuko chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambaye kituo chake ni Nzega.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Thomas Masese, alisema hawana utaratibu wa kukusanya fedha taslimu bali wanapokuwa wakifanya kazi mbalimbali ikiwamo tathmini ya kuhamisha umiliki wa mali.




Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa jengo kwa ajili ya kusimika mashine ya kukamua mafuta ya alizeti wa kikundi cha wakulima cha Changamkeni katika Kijiji cha Masinono, Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, Albert Ochare, akikagua mashine hiyo baada ya kukabidhiwa na Shirika la Maendeleo ya Kilimo na Ufugaji Musoma (SHIMAKIUMU), juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# WMA yahimiza mizani kuhakikiwa

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

VIONGOZI wa vyama vya msingi vya ushirika mkoani Lindi, wametakiwa kuhakikisha mizani inayotumiwa katika ununuzi wa mazao inahakikiwa na kuwekewa alama maalumu za Wakala wa Vipimo (WMA).

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Tawala Mkoa wa Lindi, Rehema Madengea, wakati wa mafunzo yaliyotolewa na WMA kutokana na msimu wa ununuzi wa mazao unakaribia kuanza.

Rehema aliwaambia wafanyabiashara na viongozi wa vyama vya msingi kuwa wizi wa aina yoyote ni kosa la jinai hivyo hata kuibia wananchi na wakulima kwa kuchezea vipimo ni kosa la jinai na yeyote atakaye kamatwa kujihusisha na vitendo vya uchezeaji wa vipimo atakamatwa na kuchukuliwa hatua stahiki.

"Nawasihi sana wanunuzi wa mazao kuacha kutumia vipimo batili kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwanyonya wakulima ndiyo maana wafanyabiashara wanaendelea kwa kasi huku wakulima wanabaki katika hali duni ya kiuchumi," alisema Katibu Tawala.

Kadhalika, Rehema Madenge ameupongeza Wakala wa Vipimo kwa kuendelea kupanua wigo wa kazi za vipimo katika maeneo mapya na kwa sasa taasisi hiyo inafanya uhakiki wa dira za maji pamoja na mita za umeme na kwa kuzingatia hilo Rehema ameagiza Mamlaka ya maji Mkoa wa Lindi (LUWASA), kuhakikisha wateja wote wapya na wa zamani wanafungiwa mita za maji zilizohakikiwa na Wakala wa Vipimo na kuwekewa alama maalumu ambayo ni lakiri (seal).

Akizungumza na mwandishi wetu, Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Lindi, Andrew Mbwambo, alisema kuwa Wakala wa Vipimo unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura na. 340 na mapitio yake mbalimbali na kwamba mizani ya wafanyabiashara wadogo na inayotumika katika vyama vya msingi vya ushiriki kwa kawaida hufanyiwa uhakiki mara moja kwa mwaka na baada ya kumaliza ukaguzi mbalimbali za kushtukiza hufanyika katika maeneo hayo ili kujiridhisha kama vipimo vinatumika kwa usahihi kama vilivyohakikiwa awali.

Meneja Mbwambo amewaonya wafanyabiashara na viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika kujiepusha na vitendo vya uchezeaji wa vipimo kwa lengo la kutaka kujipatia faida zaidi kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha Sheria ya Vipimo Sura na. 340 na mapitio yake mbalimbali ambayo inaeleza adhabu kwa mtu atakaye kutwa amechezea vipimo ni faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 20,000,000 inategemea na ukubwa wa makosa.

Vilevile, wakati wa mafunzo wafanyabiashara na viongozi wa AMCOS walielezwa madhara mbalimbali yatokanayo na matumizi yasiyo sahihi ya vipimo ambayo ni pamoja na kukiuka Sheria ya Vipimo ambayo inaweza kusababisha mfanyabiashara au chama cha ushirika kuadhibiwa kwa kulipa faini au kupata adhabu ya kifungo mahakamani na mali yake kutaifishwa.

Pia kumwibia mteja kwa kumpunja ni moja wapo ya wizi na ni kinyume na maandiko ya vitabu vitakatifu, lakini vile vile biashara zinaweza kufa ama kufilisika kwa kuzidisha bidhaa kwa wateja bila kutumia vipimo vilivyo sahihi katika biashara.

# Matumizi mtandao kufikia asilimia 80 mwaka 2025

SERIKALI imesema imeweka mikakati ya matumizi ya mtandao kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2025.

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Halima Mdee.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali katika kuhakikisha Watanzania wanapaka huduma ya intaneti ili washiriki dunia ya TEHAMA na kidijitali.

Naibu Waziri Kundo alikiri kuwa asilimia kubwa ya Watanzania hawatumii data na kwa sasa serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha intaneti inapatikana kwa wananchi.

"Mkakati uliopo ni kuhakikisha matumizi ya intaneti yanaongezeka hadi kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2025 kutoka asilimia 43 ya sasa," alisema Kundo.

Katika swali la msingi la Mbunge wa Igalula (CCM), Daud Venant, alitaka kujua mpango wa serikali wa kupeleka mawasiliano ya simu kwenye vijiji vya Igalula ambavyo havina mawasiliano ya simu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kundo alisema serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ina jukumu la kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote ya vijijini na mijini yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara.

Alisema hadi sasa kata 686 zimefikiwa na huduma za mawasiliano nchini na ujenzi wa minara ya mawasiliano unaendelea katika kata 371.

"Igalula kuna kata 11, ambapo serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imetekeleza miradi sita ya mawasiliano Igalula, ambapo imejengwa minara sita inayotoa huduma za mawasiliano katika kata tano ambazo ni Kizengi, Loya, Lutende, Miswaki na Tura," alisema Kundo.

Alifafanua kuwa kata zenye watoa huduma za mawasiliano Igalula ni 10 ambazo ni Igalula, Kigwa, Loya, Lutende, Miswaki, Kizengi, Miyenze, Tura, Goweko na Nsololo.

"Pamoja na jitihada hizo za serikali, Kata ya Mmale na baadhi ya maeneo ya kata za Jimbo la Igalula japo yana watoa huduma bado yanalalamikiwa kuwa yana changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano, serikali kupitia UCSAF itavifanyia tathmini vijiji vyote vya Igalula.

# Mbunge aomba waathirika vurugu uchaguzi kulipwa

MBUNGE wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka, ameiomba serikali kuwalipa kifuta machozi wakazi wa Liwale walioathirika na vurugu za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema yeye ni miongoni mwa waathirika wa vurugu hizo, kwamba alipoteza mali zenye thamani ya Sh. milioni 301.5 ambazo zilichomwa moto.

"Kuna nyumba zaidi ya sita zenye thamani ya Sh. milioni 417.3, magari nane yenye thamani ya Sh. milioni 299.7, pikipiki nane zenye thamani ya Sh. milioni 22.1, vifaa vya ndani Sh.milioni 145.1, uharibifu huu umeigharimu halmashauri yetu Sh. milioni 886," alisema Kuchauka.

Alihoji serikali haioni umuhimu kwa wananchi hawa waathirika zaidi ya 15 kuwashika mkono kuwapa kifuta machozi.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, alikiri serikali kupata taarifa za kutokea kwa vurugu zilizosababishwa na wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale na kuleta uvunjifu wa amani, uharibifu wa vitu mbalimbali ikiwamo mali za wananchi na serikali. "Uhalifu huo umefanyika wakati wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, 2020 katika Jimbo la Liwale na maeneo mengine mkoani Lindi. Aidha, serikali ilifanya jitihada mbalimbali za kumaliza vurugu hizo kwa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa sheria za nchi, kufanya vurugu za aina hiyo ni kosa la jinai.

"Matokeo ya madhara ya vurugu hizo yatashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusu masuala ya makosa ya jinai, Sheria ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2015 na kanuni zake za utekelezaji hazina ufungamanisho wa pamoja na madai ya kijinai na hasa yahusuyo uharibifu wa mali na namna ya kulipa fidia," alisema. Aidha, alitoa wito kwa kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa wa Lindi kuhakikisha uchunguzi kuhusu vurugu hizo unakamilika na hivyo kulifikisha suala hilo katika vyombo vya sheria, ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

"Napenda kuwapa pole wale wote walioathirika na vurugu hizo na kuwaomba wananchi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili kudumisha amani na usalama nchini," alisema.

Katambi alisisitiza wananchi kufuata sheria na kanuni huku akisema wakati wa uchaguzi matukio hayo ya kihalifu yamekuwa yakitengenezwa na kupongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa hatua ilizochukua.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka (kushoto) na Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mfuko kuwasaidia wanawake, wafanyabiashara waanzishwa

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama, amesema serikali imeanzisha mfuko utakaosaidia shughuli za wanawake na wafanyabiashara wadogo na kati, ili kufanya biashara kubwa ikiwamo uwekezaji kwenye viwanda na madini.

Aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Same Mashariki (CCM), Anne Kilango.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kinamama wa Same wapo kwenye machimbo ya Jasi na kuitaka serikali ione umuhimu wa kuhakikisha wanapata mikopo maalum.

Kwenye swali lake, Mbunge Kilango alihoji: "Uchimbaji wa jasi unachukua fedha nyingi, serikali haioni umuhimu wa kuwapa mikopo kinamama wote Watanzania wanaochimba madini?"

Akitoa majibu ya nyongeza ya swali hilo, Waziri Mhagama alisema kupitia mpango maalumu wa serikali umeanzishwa mfuko huo.

"Kwa hiyo ninawaomba sana waheshimiwa wabunge mnaweza kuwasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili mpate taarifa ya mfuko huu kinamama na Watanzania wengine waanze kutumia," alisema Mhagama.

Alisema tayari mfuko huo umeshakuwa na fedha na umeshaanza kutumika kufanya uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Awali, akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, alisema lengo la serikali kujenga barabara ya Makanya ni kuwainua kinamama wanaochimba kwenye machimbo ya jasi.

Silinde alisema: "Katika moja ya sheria zilizotungwa na bunge ni kuhakikisha asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri zinakwenda kwa makundi ya kinamama, vijana na watu wenye mahitaji maalum, Mheshimiwa mbunge ushauri wako serikali utachukua na kufanyia kazi."




**Habari zote na Augusta Njoji**



Ukurasa 14

**Naibu Waziri Katambi anavyochimbua ilikojikita OSHA, afya, usalama kazini**



Ukurasa 13

Namna EWURA ilivyoamua kuzibana Mamlaka za Maji zinazobambika bili



Ukurasa 12

**LICHA USHINDI WA MKOA...**

**Kuendekeza mila zaidi kunawafanya wafugaji Kiteto wasiachane na malaria**

## DK. LEONARD MABAI:

# Mwanza tunakikabili hivi kichocho, ugonjwa 'pasua kichwa' Kanda Ziwa

• Kimyakimya imefikia milioni 22 nchini

**Na Yasmine Protace**

UGONJWA wa kichocho sio jina geni. Umekuwa ukisumbua sana kwa watu wanaoishi katika maeneo ya mwambao, baharini, kwenye mito na maziwa.

Hivyo, watu wanaoishi katika maeneo hayo wapo katika hatari ya kupata magonjwa hayo. Kimsingi, kichocho sio jina geni na umekuwa ukienezwa kwa umma kwa njia ya maji.

Kwa jamii iliyoko pembezoni mwa bahari, mitoni na kwenye maziwa, wanatakiwa kuwa makini dhidi ya maambukizi yake.

Umakini unachukua nafasi kwa kujizuia kuogelea kuchezea maji hayo. Kimsingi, ni njia ya kujizuia kupata maambukizi ya maradhi hayo.

Athari ya minyoo tumbo inaambukizwa kwa njia ya chakula kilichoathiriwa na kinyesi chenye mayai ya minyoo, hivyo mtu anatakiwa kuwa makini asipate maambukizi ya kichocho.

Mratibu wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTD) Mkoa wa Mwanza, Dk. Mabai Leonard, anataja kuna kadirio la Watanzania milioni 22 wanauogua kichocho.

Anasema katika idadi hiyo, Kanda ya Ziwa inaongoza kuwa na maambukizi kati ya asilimia 50 hadi 80 ya magonjwa hayo yaliyokuwa hayapewi kipaumbele.



Mazingira rafiki yanayohamasisha kuenea maradhi ya kichocho. **PICHA: MTANDAO**

Dk. Mabai anasema kwamba, kichocho na minyoo ya tumbo bado ni tatizo kubwa mkoani humo na ili kukabiliana na tatizo hilo, Mwanza imeandaa kampeni kutoa kingatiba kwa watoto wenye umri wa kwenda shule.

Hao ni wenye umri kuanzia miaka minne hadi 15 kwa shule za msingi zote, inayoendana na kutengwa fedha Sh. 288,474,400 kwa ajili ya kazi hiyo.

Aidha, anaongeza kuwa kichocho na minyoo ya tumbo, hazina dalili za haraka kabla ya kupata matibabu, hivyo utoaji kingatiba unalenga kudhibiti na kutibu magonjwa hayo kwenye jamii.

Hata hivyo, anasisitiza kuwa halmashauri zote mkoani Mwanza zihakikishe watoto watakaopewa kingatiba wamepata chakula saa mbili kabla ya kumeza.

Anazitaja kingatiba hizo, ni dawa aina ya albendazole kwa ajili ya minyoo tumbo na prazequantel ya kichocho. Dk. Leonard anaendelea:

Anayaeleza kuwa mazingira hatarishi kwa wananchi wake kupata magonjwa hayo, huku Profesa Humphrey Mazigo wa Chuo Kikuu Katoliki cha Sayansi na Tiba za Afya Bugando (CUHAS), anataja kuwapo jamii masikini vijijini zinavyoathiruwa na jumla ya magonjwa 17.

Profesa Mazigo, anajumuisha kichocho katika orodha yake, pia minyoo ikiwa sehemu ya orodha ya maradhi sumbufu katika ukanda wa kitropiki penye jamii masikini, zinazoishi kwa gharama chini ya dola mbili za Kimarekani (Sh.4,600), hazina uwezo wa kugharamia tiba na kuathiri uwezo wa watoto kwenda shule.

"Tanzania ni moja ya nchi zilizoathiriwa na ugonjwa wa kichocho hasa Bonde la Ziwa Victoria na hasa wakulima, wavuvi na watoto na kuna watu bilioni mbili duniani wameathirika na minyoo ya tumbo.

"Zaidi ya watu milioni 300 wameathirika sana, huku 155,000 kila mwaka duniani hufariki kutokana na magonjwa hayo," anasema Profesa Mazigo.

Kaimu Mratibu wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, Oscar Kaitaba, anasema kuna magonjwa yanayosababisha madhara kwa binadamu, ikiwamo ya kudumu, kuathiri maendeleo na makuzi ya watoto, kuwapunguzia uwezo wa utendaji na kuisababishia jamii umasikini.

Licha ya kuwapo magumu ya mafanikio katika utoaji kingatiba kwenye halmashauri 184 nchini, ambao kiwango cha maambukizi kimepungua kwenye halmashauri 71, bado kuna halmashauri sita.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alipofungua Kikao Kazi Cha Uhamasishaji wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele yaliyofanyika Jijini Mwanza, anasema ongezeko lake linapunguza utimamu wa afya ya jamii na kusababisha familia kutumia rasilimali nyingi, kukabiliana na magonjwa hayo.

AFYA

LICHA USHINDI WA MKOA...

# Kuendekeza mila zaidi kunawafanya wafugaji Kiteto wasiachane na malaria

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

- Ishara chanya; 'angalau' waendao kliniki
- Kwingineko maambukizi hayafiki asilimia 1

MWISHO wa mwezi uliopita kuliadhimishwa Siku ya Malaria Duniani yenye kaulimbiu isemayo "0 Malaria inaanza na mimi."

Katika tathmini hiyo mkoani Manyara, ambako kiwango cha maambukizi yako chini ya asilimia moja, Nipashe iliamua kumtafuta Mratibu wa Malaria mkoani, Evance Simkoko, kurejea maadhimisho hayo ya Aprili 25 mwaka huu.

Simkoko anajigamba kwamba inazuilika ikiwa ni tatizo linaloingiza familia nyingi katika gharama kubwa ya tiba, huku serikali nayo inatumia fedha nyingi kwa eneo hilo

**CHANZO MALARIA?**

Mratibu huyo anasema, chanzo cha ugonjwa malaria ni mdudu mbu anayechukua wadudu wadogo, anayempa mtu asiye na vimelea vya ugonjwa huo.

Anasema, malaria inashambulia makundi yote ya binadamu, ila kuna watoto wenye umri chini ya miaka mitano, ndio wanaathirika sana kutokana na kinga yao ya mwili inakuwa iko chini, hivyo kusababisha vijidudu kuingia kiurahisi mwilini.

Mtaalamu huyo anasema, kung'atwa na mbu ni chanzo kikuu cha binadamu kuambukizwa na ugonjwa huo.

Kiongozi huyo wa afya anasema, hali ya mkoa maambukizi yako chini ya asilimia moja isipokuwa Wilaya ya Kiteto na Simanjiro, maambukizi yanazidi asilimia moja kutokana na hali ya hewa kubadilika.

Simkoko anasema mara nyingine maambukizi yanafikia asilimia tatu, huku akihusisha hali hiyo na kuwa jirani na Mkoa wa Tanga, ambao maambukizi yako juu.

Licha ya mbu kuambukiza ugonjwa huu anataja vyanzo vingine kuwa ni kutokufyeka vichaka, uwepo wa madimbwi ya maji ambayo yanazalisha mbu,

Vipande vya vyungu vilivyopasuliwa na vifuu vya nazi ambavyo uhifadhi mazalia ya mbu kutokutumia vyandarua na matumizi ya dawa pasipo vipimo vilivyodhibitishwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pia Shirika la Afya Duniani (WHO).

Ili kuzinusuru baadhi ya wilaya, serikali ilitoa vyandarua kwa zaidi ya kaya 50,000 wilayani za Kiteto na Simanjiro, vyandarua kaya 60,000.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alipozungumza katika Siku ya Malaria Duniani mwezi uliopita. **PICHA: MTANDAO**

> **Mara nyingine maambukizi yanafikia asilimia tatu, huku akihusisha hali hiyo na kuwa jirani na Mkoa wa Tanga, ambao maambukizi yako juu.**

Katika kuhakikisha watoto chini ya miaka mitano na wajawazito anasema serikali ina mpango wa kugawa vyandarua kwa wajawazito bure kwa hudhurio la kwanza la mjamzito, anapotimu wiki ya 12.

Pia, watoto nao wanapewa vyandarua wakienda kwenye chanjo ya miezi tisa na wanafanya hivyo, kwa imani vyandarua vinavyotolewa kwa mama mjamzito, vinakuwa vimeshachakaa.

Mratibu Malaria anasema, matarajio yaliyoko mwaka huu ni zaidi ya watoto 50,000 watawapatia vyandarua, kupitia vituo vyote vya huduma za afya mkoani humo.

**WANAVYODHIBITI MALARIA**

Simkoko anasema, kumdhibiti mbu huanzia ngazi ya kukiua kiluilui na kumwepusha kuendelea kuzaliana, sambamba na upulizaji dawa.

Njia nyingine anaitaja kuwa ni kulala ndani ya vyandarua vyenye dawa, kupiga dawa kwenye maji na watu wanaweza kuendelea kuyatumia bila kupata madhara(Ukoka), kufyeka vichaka na kufanya usafi wa mara kwa mara kwenye mazingira.

**HALMASHAURI VITANI**

Anasema, serikali imeweka halmashauri tano za mkoa Manyara, kwenye mpango wa utokomezaji, akizitaja kuwa ni: Mji Babati Mji; Mji wa Mbulu; wilaya za Kiteto, Mbulu, Hanan'g na Babati.

Simkoko anasema kazi ya halmashauri hizo ni kuwapima wagonjwa wanaowapokea na kuwafatilia kudhibiti maambukizi.

"Mpango huu wa kutokomeza malaria, wagonjwa wengi tunaowapima tunakuta wamesafiri kutoka Simanjiro au Kiteto," anaeleza Simkoko

Mtaalamu huyo wa afya, anasema baada ya kuwabaini wanawafanyia vipimo vinavyotambuliwa na Wizara inayohusika na Afya, pia Shirika la Afya Duniani (WHO) na kuwasisitiza kupata matibabu sahihi.

Anakiri kuwapo ushirikano wa kiserikali, kwa kutengewa fedha za mafunzo kwa wataalamu wa afya, pia kugawa vyandarua bila malipo kwa kaya zaidi ya 100,000, hali kadhalika kuwekewa miongozo ya kuudhibiti ugonjwa.

**VIKOJE VIKWAZO?**

Mratibu anakiri kuwapo tatizo, baadhi ya watu hawafuati taratibu wanazowaelekeza katika kudhibiti ugonjwa, ikiwamo kutofyeka vichaka, kuzagaa vifuu vya nazi na vipande vya vyungu vilivyopasuliwa, vivyo hivyo kuna wasiotumia vyandarua.

Wakati wastani wa vifo vya watoto na wajawazito viko chini ya asilimia moja Manyara, Mratibu Malaria ansisitiza hatua za kutumika dawa kinga za hospitalini, kuvaa nguo ndefu zenye mikono mirefu, vyote vikisaidia kuzuia mbu na kwa wanaoshinda nje ya majumbani, wapake mafuta ya kuua mbu.

Kaimu Mratibu wa Malaria wa Halmashauri ya Wilaya Babati, James Mleli, ambaye pia ni Mratibu wa Chanjo, anasema katika eneo lake, kiwango cha maambukizi ni asilimia 0.4, ingawaje hakutaja idadi ya wagonjwa

**WAATHIRIKA MALARIA**

Mkazi wa wilayani Kiteto, Mohamed Shaban, anasema malaria kwao bado ni tatizo kubwa na chanzo chake ni mazingira kutofanyiwa usafi wa kukata miti na mambo ya kusafisha mazingira yanayohamasisha mbu.

Shaban anasema, wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusu kujikinga katika eneo hilo, ambalo sehemu kubwa ni ya wafugaji, penye madimbwi mengi yanayozalisha mbu hayajafukiwa.

Katika athari hiyo, anawataja watoto wenye umri chini ya miaka mitano ndio waathirika wakubwa kwa sababu ya kukosa ulinzi imara wa miili yao, akitoa mfano kutoka maisha ya wafugaji, mavazi yao baadhi hayajasitiriwa vizuri, inakuwa rahisi mbu kuwang'ata.

Anafafanua, walau sehemu kubwa ya wanaopata elimu hiyo hasa kwa wafugaji wa Kiteto ni kinamama wajawazito, kupitia darasa la kliniki.

Mkazi mwingine wa Kiteto, Halima Juma, anasema kuna familia zilizopata vyandarua, ila zina tabia ya kupuuza ushauri wanaopewa, ingawaje serikali inaendelea kuwaelimisha pasipo kuchoka.

**TATIZO LA WAFUGAJI**

Halima anataja shida ya jamii ya wafugaji, ni kutoamini mageuzi na maboresho ya kisasa, yanayokinzana na mila zao, hawaamini iwapo elimu itolewayo ina nafasi ya kutokomeza ugonjwa huo.

Anataja tatizo jingine, ni watu kukaa mifugo muda mwingi, mbu wanaowaegemea mifugo, hihamia kwa binadamu.

Batholomayo Mwiru, anayeishi Kwere, Babati anasema malaria inaongoza kuwasumbua kiafya, ikifuatiwa na homa ya matumbo (typhoid0 na waathirika wakubwa ni watoto wenye umri chini ya miaka mitano, pia wajawazito.

Mwiru anaishauri serikali ichukue hatua ya kuingilia kati kupambana na mifumo ya maisha kwa kutunza mazingira na kuimarisha upatikanaji kwenye vituo vya tiba.

Takwimu za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni maradhi yanayoua kila mwaka wastani wa watu 100,000 nchini, malaria inasababisha ugonjwa figo na ina wadudu wa chembe nyekundu za damu zinazojulikana kitaalamu'red blood cells.'

**HALI YA DUNIA**

Kwa mujibu wa WHO, zaidi ya watu 400,000 hufariki kila mwaka kwa malaria. Pia, kuna wastani kila baada ya dakika mbili kuna mtoto anafariki duniani, kutokana na marashi hayo.

Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), kwa kushirikiana na wizara inayohusika na ya afya, nchini, linasema kuna ahueni baada ya kugawa vyandarua maalum vilivyotengenezwa vimenyunyiziwa dawa ya kuua mbu.

MAZINGIRA

AGIZO LA WAZIRI AWESO...

# Namna EWURA ilivyoamua kuzibana Mamlaka za Maji zinazobambika bili

• Yakiri udhaifu wasomaji na mita zao • Rungu laja maeneo 24, wakuu wake

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SUALA la ubambikizaji ankara za maji limekuwa tatizo sugu kwa baadhi ya mamlaka za maji nchini, hali inayochangia kuibuka malalamiko ya aina hiyo kila mara kutoka kwa wananchi.

Kati ya Mei 6 hadi 10 mwaka huu, kwenye mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji bungeni mwaka wa fedha mpya, suala hilo liliibuliwa katika mjadala huo kati ya Alhamisi wiki iliyopita na Jumatatu wiki hii.

Wabunge walitaka serikali kuchukua hatua kushughulikia kero hiyo, kwa kuwa inawaumiza wananchi.



Mradi wa maji ulioko Nguruka, unaohudumiwa na Mamlaka ya Maji Kigoma. Anayeukagua ni Waziri wa Maji, wakati huo akiwa naibu waziri katika wizara hiyo. **PICHA: MTANDAO**

### JICHO LA WAZIRI

Hata hivyo, wiki kadhaa kabla ya uwasilisho bungeni, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kusitisha upandishaji ankara mpya za maji zilizopaswa kuanza kutozwa Januari mwaka huu.

Anakiri kuwapo ubambikizaji ankra na akakemea tabia ya watumishi wa mamlaka za maji kusoma mita bila kuwashirikisha wateja, huku wanafikia hatua ya kukadiria bei.

"Kuna baadhi ya mamlaka ambazo zimekuwa zikitoa bei ya maji bila kuidhinishwa na EWURA. Naagiza EWURA kuhakikisha mnawajengea uwezo wakurugenzi na kutoa elimu kwa wananchi.

"Ili kujua kujua wapi kwa kwenda wanapokuwa na malalamiko, ikiwamo ya kutokubaliana na bili ya maji iliyotolewa," anasema.

Kwa kutumia mamlaka yake kisheria kudhibiti bei, ada, tozo katika huduma za nishati na maji, EWURA katika utekelezaji agizo la Waziri Aweso, ilichunguza na kubaini mambo 11 yanayohusu malalamiko ya ankra za maji.

### 'MADUDU' KUIBULIWA

Malalamikio mengi yaliangukia kubambikiwa bili, usomaji mita usiokuwa shirikishi na ukataji maji pasipo kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa, hata EWURA ikasitisha mabadilko ya bei kwa mujibu wa agizo la waziri, kujipa nafasi ya kuchunguza malalamiko hayo

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, anasema baada ya kusitisha utozaji bei mpya za maji zilizopaswa kuanza Januari mwaka huu, walifanya ukaguzi maalum katika mamlaka za maji 24 kati ya 94 zilizopo.

> **Baadhi ya mamlaka kutoza bili za maji kwa kufanya makadirio, kutokana na kuharibika kwa mita za maji. Mfano, Mamlaka ya Tanga imeonekana inapeleka bili za makadirio kwa wateja.**

Anazitaja mamlaka zilizofanyiwa ukaguzi ni Kigoma, Bukoba, Babati, Moshi, Arusha, Tanga, Geita, Shinyanga, Kahama, Dodoma, Musoma, Mbeya, Njombe, Songea, Vwawa-Mlowo, Mugango-Kiabakari, Bunda, Makambako, Sengerema, Muleba, Mwanhunzi, Gairo na Ngara.

### KILICHOBAINIKA

Mkurugenzi Chibulunje, anasema baada ya uchunguzi, EWURA ilibaini udhaifu katika usomaji mita ambao baadhi ya wasomaji wanakosa umakini kutekeleza jukumu lao, hali iliyodhihirika katika mamlaka zote 24.

"Mamlaka ya Maji Kigoma ndio wanaongoza kwa kubambikizia bili ambayo asilimia 80 ya malalamiko yanahusu bili za maji," anasema Chibubulunje na anaongeza:

"Kingine kilichobainika ni udhaifu katika mita za maji. Baadhi zilibainika kutofanya kazi kwa ufanisi baada ya kuhakikiwa na Wakala wa Vipimo na Mizani(WMA).Tatizo hili limejionyesha zaidi kwa Mamlaka ya Maji Iringa na Dodoma.

"Baadhi ya mamlaka kutoza bili za maji kwa kufanya makadirio, kutokana na kuharibika kwa mita za maji. Mfano, Mamlaka ya Tanga imeonekana inapeleka bili za makadirio kwa wateja."

Mhandisi Chibulunje anadokeza kuwapo uzembe wa baadhi ya mamlaka za maji, katika usimamizi wa bei zinazotozwa kwa wateja, kiwapo utozaji bei zaidi ya zilizoidhinishwa na EWURA.

Hapo katika orodha ya zinazohusika lawama, zimo mamlaka za Mbeya, Makambako, Songea, Tanga, Iringa, Shinyanga, Kahama, Geita, Arusha, Moshi, Babati, Ngara na Kigoma.

Pia, baadhi ya mamlaka zinalalamikiwa kuendelea kuwa na wateja wasio na mita, matokeo yake wanatozwa bili zisizoendana na matumizi. Kuna malalamiko kwamba, ankara za wateja hazitoi taarifa za kutosha kwa bei inayotozwa.

"Kutozingatia utaratibu wa kutoa taarifa kwa wateja, inapotokea kuwapo kwa mgawo wa maji, hivyo kuleta usumbufu kwa mteja.Baadhi ya mamlaka hutoza wateja bei wasizostahili kulingana na makundi yao, utekelezaji hafifu wa miradi inayotekelezwa kutokana na fedha zilizoidhinishwa katika maagizo ya bei," anasema.

### HATUA ZA EWURA

Chibulunje anasema kutokana na matokeo hayo, wamechukua hatua kadhaa, ikiwamo kutoza faini ya Sh.500, 000 kwa mamlaka za maji Tanga na Babati, zilizobainika kuwauzia wananchi maji bei isiyoidhinishwa na EWURA.

Pia, anasema EWURA imeziagiza mamlaka kuwafidia wateja waliotozwa bili za maji zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa.

"EWURA imezipelekea maagizo mamlaka za maji za Mbeya, Songea, Makambako, Mwanhuzi na Gairo, zijieleze kwanini zisichukuliwe hatua stahiki kwa kukiuka maagizo ya EWURA

### RUNGU LA KIUFUNDI

Anabainisha kwamba EWURA imezitaka mamlaka zote kupima ufanisi wa mita zao za maji, kuwa na miundombinu ya kupima ufanisi wa mita za wateja wake zilizohakikiwa na Wakala wa Vipimo, kabla ya kuwafungua wateja.

Mamlaka hiyo pia imeagizwa kufuatilia ufanisi wa mita hizo kila baada ya miaka mitano, ikiendana na wateja kutumiwa taarifa za usomaji mita, kabla na kupewa muda wa kuhakiki na kisha ndio panapo muafaka, ankara husika zitolewe.

EWURA katika uamuzi wake mzito utokanao na agizo la Waziri Aweso, inatarajiwa kuwasilisha kwa mamlaka ya uteuzi majina ya mamlaka za Babati, Kigoma na Tanga zuinazotajwa kuwa sugu kushindwa kutatua malalamiko ya wateja, ili hatua za kinidhamu zichukuliwe.

Anasema, sheria iliyounda EWURA inaipa mamlaka ya kupendekeza msimamizi mwingine, sambamba na hatia nyinginezo kisheria , zikiwamo za watu kifikishwa mahakamani, pale imapothibtika mazingira ya kufanya hivyo

Chibulunje anasema, EWURA itaendelea kuchunguza mamlaka zingine zilizobaki na kuchukua hatua stahiki.

Kaimu Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira EWURA, Mhandisi Titus Safari, anasema sheria iliyoiunda inagusa kuidhinisha bei za maji na kuhakikisha huduma za maji zinatolewa na mamlaka za maji nchini.

Katika kufanya hivyo, anasema wanazingatia matakwa ya sheria, kanuni na miongozo inayotolewa kwa lengo la kutoa huduma bora ya maji kwa umma.

Ni udhibiti ambao pia, unahakikisha ankra za maji wanazotozwa watumiaji zinazingatia bei iliyoidhinishwa na EWURA; kunakuwapo usahihi katika mita za maji zinakokotolewa vilivyo kwa maslahi ya wananchi kwa ujumla.

AFYA

# Naibu Waziri Katambi anavyochimbua ilikojikita OSHA, afya, usalama kazini

**Na Anthony Gervas,** Mwanza

KILA Aprili 28 ya mwaka duniani kunakuwapo maadhimisho Siku ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi, mwaka huu kitaifa yalifanyika kwenye Uwanja wa Michezo wa Nyamagana, jijini Mwanza chini ya uratibu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

Maadhimisho hayo nchini lengo lake kubwa ni serikali kuhakikisha inaendeleza kampeni kuhamasisha mazingira salama kwa wafanyakazi kazini, pia maslahi yao.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,Vijana na Ajira (mwenye suti nyeusi), Katambi Patrobass, akipata ufafanuzi kutoka kwa wafanyakazi katika mabanda yao. Kulia aliyeambatana naye ni Kaimu Mtendaji Mkuu, Khadija Mwenda. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

### NAIBU WAZIRI KATAMBI

Naibu Waziri,Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Katambi Patrobass, anaeleza namna maadhimisho hayo yanayosimamiwa na taasisi hiyo ya OSHA nchini, akisema:

"Maadhimisho hayo kwa serikali yamelenga kuangalia maslahi mapana na haki za msingi za wafanyakazi nchini na kuzungumzia mstakabali wa sera na sheria zinazohusu masuala ya wafanyakazi kazini."

Anafafanua kwamba licha ya serikali kutekeleza hayo, lengo ni kuhakikisha inaendeleza kampeni kuhamasisha uwapo wa mazingira salama kazini na kuepuka ugumu kazini, unaozaa mazingira hatarishi.

Tangu yaanze rasmi nchini mwaka 2004, maadhimisho hayo ya kila Apriil 27 kitaifa hadi ni miaka 17. Mwaka jana hayakufanyika kutokana na janga la corona.

Naibu Waziri anasema wameweza kuwashirikisha wadau na vyama vya wafanyakazi, vikiwamo TUCTA, TALGWU na Chama cha Waajiri (ATE), kampuni za dini, mifuko ya hifadhi ya jamii, zikiwamo NSSF na PSSF.

Vilevile, anasema kuna mustakabali wa kutolewa mafunzo ya usalama wa afya kwa wajasiriamali wenye sekta rasmi na zisizokuwa rasmi wapatao 800, zilizoenadana na kutolewa tuzo kwa wafanyakazi bora walionufaika.

Wengine wanaotajwa ni waendesha bodaboda na makundi ya wenye ulemavu kutoka Kanda ya Ziwa, Geita, Mara na Mwanza.

### KAMPUNI SUGU

"Kampuni zitakazobainika kutolipa mishahara ya wafanyakazi kwa wakati, kutopeleka makato yao ya kujiwekea mafao ya akiba kama vile mifuko ya NSSF.

> **Tutayaweka kwenye orodha ya wadaiwa sugu na kuyatangaza katika gazeti, la sivyo yajisalimishe mapema katika ofisi ya Katibu Mkuu.**




Banda la Maonyesho la Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi(OSHA), katika maadhimisho yake yaliyofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyamagana, jijini Mwanza.

"Tutayaweka kwenye orodha ya wadaiwa sugu na kuyatangaza katika gazeti, la sivyo yajisalimishe mapema katika ofisi ya Katibu Mkuu," anatamka Naibu Waziri Patrobass.

Anakiri mkakati wake ni kufuata nyayo za Rais Mama Samia Hassan, anayesimamia kauli mwongozo yenye msimamo "Ukinizingua, tutazinguana."

### KAZI IKOJE?

Naibu Waziri Patrobass anawaonya viongozi na waajiri wasiwanyime wafanyakazi fursa za kufanya mikutano au vikao vilivyowekwa kisheria, kwani ni kukiuka taratibu za utoaji haki kwao.

Patrobass anawapa nafasi wanachama wa vyama vya wafanyakazi kupeleka taarifa na majina ya waajiri au viongozi wanaofanya hivyo kwa katibu mkuu, ili kudhibiti tabia hiyo, kwani wapo baadhi wanaofanya kazi kwa maslahi binafsi.

Anasema, kila kipindi duniani kuna wafanyakazi zaidi ya milioni 2.3 wanaopoteza maisha kutokana na ajali kazini na milioni tatu wanaojeruhiwa, huku serikali kupitia OSHA, inawajibika kuwahakikishia usalama kiafya ili walitumikie taifa.

### MAREKEBISHO YA TOZO

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, anafafanua taasisi hiyo imeshafanya marekebisho ya sheria ya afya na usalama kazini.

Anasema, wameondoa tozo mbalimbali zikiwamo za ada ya usajili eneo la kazi iliyotozwa kati ya Sh.50, 000 hadi Sh. 1,800,000.

Khadija anasema, ada ya fomu za usajili sehemu ya kazi iliyotozwa Sh. 2,000 na faini zinazohusiana na vifaa vya kuzimia moto ya Sh.500, 000, ziliingiliana na taratibu zinazosimamiwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Tozo nyinginezo zilizoondolewa na OSHA ni Sh. 200,000 ada ya afya na usalama kila mwaka; ushauri wa kitaalamu wa usalama na afya iliyokuwa Sh.450, 000 kwa saa kwa mtaalam mmoja. Kwa sasa, ada iliyobaki ni Sh.120, 000.

### MAGUMU YALIYOBAKI

Mwenda anasema, hadi sasa kuna changamoto za kuwalinda wafanyakazi kuhusu haki zao, kuhakikisha hawabaki kwenye mazingira hatarishi, ikiwamo ajali na ama kuwapotezea maisha au kujeruhiwa.

Anaeleza tafiti zilizofanyika mwaka 2019, zinaonyeshwa wafanyakazi wengi wanaopata ajali na kujeruhiwa kazini katika sekta mbalimbali ikiwamo ya uzalishaji, ujenzi na migodini ni wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 35.

### YALIYOBAKI?

Moja ya majukumu ya msingi yanayotekelezwa na taasisi hiyo chini ya sheria, ni pamoja na kukagua usalama na afya kazini na kupima afya za wafanyakazi kulingana na kazi wanazofanya.

OSHA ni taasisi ya umma iliyobeba dhamana ya kulinda usalama na afya kwa watumishi wanapokuwa kazini, kupitia usimamizi wa sheria.

Pia, inatoa mafunzo ya usalama na afya kazini, kuchunguza ajali za sehemu za kazi, kuishauri serikali kutunga sheria, sera, kanuni, miongozo na mikataba kimataifa, inayohusu usimamizi wa usalama na afya kazini.

Maonyesho hayo ni sehemu ya programu za OSHA kuongeza uelewa miongoni mwa wadau katika maeneo ya kazi na sekta mbalimbali, wakishirikiana uzoefu.

Anawakumbusha Watanzania umuhimu wa mtaji kufanyia kazi na ndio mtambo utaweza kuendeshwa sehemu ya kazi, pasipo hata uchumi na uzalishaji wake kuimarika.

Rai yake ni kuwa na uzalishaji endelevu, pia imara katika kusaidia mapato yaongezeke na wafanyakazi walipwe mishahara kwa wakati na mazingira bora kazini.



# Majaliwa aagiza kuandaliwe mitaala wahitimu kujiajiri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza kuandaliwa kwa mitaala ya elimu nchini ambayo itawezesha wahitimu katika ngazi mbalimbali kuwa wabunifu ili kujiajiri wenyewe badala ya kuendelea kukaa mitaani bila ya kuwa na kitu cha kufanya.

Majaliwa, aliyasema hayo jana wakati alipokuwa akifunga kilele cha mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU), yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema ipo haja ya kuandaliwa kwa mitaala ya elimu nchini ambayo itafanya wahitimu kuwa wabunifu badala ya kubaki mitaani bila kitu cha kufanya.

"Tuandae mitaala ambayo itafanya wahitimu wetu katika ngazi mbalimbali za elimu nchini kuwa wabunifu ili kubuni vitu mbalimbali vya kufanya waondokane na tabia ya kubaki mitaani bila kitu cha kufanya," alisema Majaliwa.

Alisema mitaala inayotumika hivi sasa inatakiwa kufanyiwa maboresho katika ngazi zote za elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo ili kuwasaidia wahitimu kuwa wabunifu.

Aliagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuimarisha maabara za kompyuta katika vyuo vya ualimu nchini ili kuwezesha kutoa idadi kubwa ya walimu watakaofundisha masuala ya sayansi na teknolojia.

"Pia bunifu zote za wabunifu nchini zinatakiwa kutambuliwa na kuendelezwa ili zitumike katika kujibu changamoto mbalimbali zilizopo katika jamii yetu," alisema Majaliwa.

Kadhalika, Waziri Mkuu Majaliwa aliagiza mamlaka zinazohusika na hatimiliki kuandaa maombi ya hati hizo na kuzipeleka katika shirika la hati miliki duniani ili kila mbunifu kuwa na haki na kitu alichobuni.

"Mpaka hivi sasa takwimu zinaonyesha kuwa sisi kama nchi tumepeleka maombi manane tu kwa ajili ya kuomba hatimiliki katika shirika hili wakati wenzetu Afrika Kusini wamepeleka maombi zaidi ya 300," alisema Majaliwa.

Vile vile, alisema anataka kuona katika mashindano ya mwaka ujao wabunifu wengi wanakuwa na hatimiliki ya vitu ambavyo wamevibuni.

"Hatimiliki ni jambo la muhimu sana watu wengi wanalia wasanii, waimbaji wa nyimbo mbalimbali hivyo mamlaka zinazohusika ziratibu maombi yote ya hatimiliki ili kuyapeka katika chombo hicho kinachotoa hatimiliki duniani na kila aliyebuni kitu chake awe na hatimiliki yake," alisema Majaliwa.

Awali Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema lengo la mashindano hayo ni sehemu ya mkakati wa kugundua na kuendeleza ubunifu nchini.

Alisema katika kipindi cha mashindano hayo kwa muda wa miaka mitatu jumla ya wabunifu 1,066 waliibuliwa na wabunifu 130 mahili wanaendelezwa na wizara.

Naye Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kufanyia marekebisho ya sheria inayosimamia mikopo ya elimu ya vyuo vikuu ili inufaishe pia na wanafunzi wa vyuo vya kati.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti cha shukrani kwa Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Said Idd, kutokana na kampuni hiyo kuwa mdhamini mkuu wa maonyesho ya Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU 2021) yaliyofanyika kitaifa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuanzisha mfuko wa umwagiliaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuanzisha mfuko wa umwagiliaji kwa ajili ya kusaidia kufufua mashamba 13 ya Wakala wa Mbegu nchini (ASA), ili kuzalisha mbegu bora kwa wakulima.

Waziri wa Kilimo Prof. Aldof Mkenda, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha pamoja na Menejimenti na bodi ya wajumbe wa ASA kuhusu uzalishaji wa mbegu bora.

Prof. Mkenda alisema hivi sasa kipaumbele cha wizara hiyo ni katika uzalishaji wa mbegu bora kupitia mashamba hayo ndio maana imejipanga kuanzisha mfuko huo.

"Tutajitahidi katika hili kwa sababu tunaanzisha mfuko wa umwagiliaji tukipata fedha tutapeleka katika miradi inayoendelea na siyo kuanzisha vitu vipya," alisema Prof. Mkenda.

Alisema itasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kutokana na kuagiza mbegu nje ya nchi na serikali itajitahidi na ASA kusimamia suala hilo.

Alisema ipo haja ya serikali kuwa msimamo unaoakisi kaulimbiu ya kilimo ni uti wa mgongo ili wakulima walime kwa tija na kuondokana na umaskini.

"Tunaweza kuwa na uchumi wa kati na hata kufikia uchumi wa juu, lakini wimbi la umaskini likaendelea kwa wananchi na tukawa tegemezi wa chakula, lakini hatuwezi kuwa na mageuzi ya viwanda bila kufanya mageuzi ya kilimo hususani katika suala la mbegu," alisema. Kadhalika, alisema ni lazima mashamba yote ya ASA yafufuliwe kwa kuwa utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi wakati mwingine hausaidii kilimo cha hapa nchini.

"Mbegu zinafanyiwa utafiti nchi nyingine, lakin zinaweza zisiendane na hali ya udongo wa Tanzania, mbegu ni usalama wa nchi, mashamba yote ya ASA yanapaswa kufufuliwa na yafanyiwe umwagiliaji, hakuna mradi mpya wa umwagiliaji utakaoanzishwa mpaka kukamilika kwa mpango huu," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya ASA, Dk. Ashura Kihupi, alisema kero kubwa kwenye sekta ya mbegu ni uwekezaji mdogo uliofanywa na serikali, mtaji mdogo kwa ajili ya kuzalisha mbegu.

Mmoja wa wajumbe wa bodi hiyo, Marco Mtunga, alisema unahitajika uwekezaji mkubwa wa mbegu. Alisema katika shamba la mbegu la Msimba, Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, hasara kubwa imetokea kwa sababu hakuna kilimo cha umwagiliaji.

# Waomba serikali bei za bidhaa mahitaji maalum kuangaliwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la utetezi wa watoto wenye mahitaji maalum Mkoa wa Dodoma, limeomba serikali kuangalia bei za vifaa saidizi kutokana na kuuzwa kwa gharama kubwa.

Katibu wa Mkoa wa baraza hilo, Janeth Sylvester, alitoa ombi hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye warsha iliyoandaliwa na mradi wa elimu jumuishi kwa ajili ya mgawanyo wa majukumu mbalimbali kwa ajili ya utetezi wa watoto hao.

Alisema gharama kubwa ya vifaa hivyo inasababisha kushindwa kumudu kuvinunua.

Alisema bado kuna haja ya serikali kuangalia vifaa mbalimbali visaidizi ambavyo gharama zake ziko juu kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Aidha, alisema watoto wengi wenye mahitaji maalumu wanaosoma watashindwa kufikia malengo yao kutokana na kutomudu kununua vifaa hivyo.

"Miongoni mwa vifaa hivyo visaidizi kwa watoto wenye ulemavu ni pamoja na mashine za nukta nundu za kuandikia moja huuzwa zaidi ya shilingi milioni mbili, huku kwa watoto wasio na ulemavu wanaotumia kompyuta huuziwa bei ya Sh. 300,000 hadi 600,000," alisema.

Aliiomba serikali kuangalia upangaji wa walimu kulingana na mahitaji ya sehemu husika tofauti na ilivyo hivi sasa.

"Serikali ihakikishe walimu wanaopangiwa kwenye shule wawe na utaalamu wa kufundisha, pia wapangiwe shule kulingana na mahitaji ya sehemu husika, bado kuna haja ya serikali kuangalia walimu hao wanaopangiwa shuleni, kutokana na baadhi yao kutokidhi vigezo katika ufundishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu," alisema.

Naye Meneja wa Mradi wa Elimu Jumuishi Tanzania Kanisa la FPCT, Suleiman Ibrahim, aliomba serikali kutenga bajeti itakayowapunguzia uchungu watoto wenye mahitaji maalum.

Suleiman alisema bado kuna tatizo la watoto wenye mahitaji maalumu walio shuleni, lakini baadhi yao wanakosa visaidizi kutokana na gharama kubwa.

Aliiomba serikali kutenga bajeti kwa ajili ya mpango wa elimu jumuishi ambao umekuwa ukisaidia katika kuboresha miundombinu mbalimbali ili iwasaidie watoto wenye mahitaji maalumu.



## Uhaba matundu ya vyoo waathiri shule Tunduma

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

SHULE za msingi katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe, zinakabiliwa na upungufu wa matundu 980 ya vyoo, hali ambayo inahatarisha afya za wanafunzi wawapo shuleni.

Kaimu Ofisa Elimu Msingi wa halmashauri hiyo, Subira Kulaga, aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa anapokea vyoo vyenye matundu 22 ambayo yamejengwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wake wa SAWA.

Alisema upungufu huo ulikuwa unahatarisha afya za wanafunzi hao kutokana na kusongamana kwenye vyoo vichache na kwamba upungufu huo ni pamoja na vyoo maalumu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

"Kabla ya UNICEF kutusaidia matundu haya Mji wetu ulikuwa na upungufu wa matundu 1012 lakini kwa sasa upungufu umebaki matundu 980, hivyo tunaomba wadau wengine wajitokeze kutusaidia kupunguza tatizo hili," alisema Kulaga. Alilishukuru Shirika hilo la UNICEF kwa msaada huo akidai kuwa umesaidia kupunguza tatizo huku akidai kuwa shirika hilo limewajengea choo cha watoto wenye mahitaji maalumu ambacho kitakuwa cha mfano.

Msimamizi wa Mradi wa SAWA, Wilhelima Malima, aliwataka walimu na wanafunzi wa shule hiyo kuvitunza vyoo hivyo ili vitumike kwa muda mrefu na kwamba kama havitatunzwa havitawasaidia kuondoa tatizo hilo.

Aliwataka wanafunzi kuvifanyia usafi wa mara kwa mara vyoo hivyo ili kulinda afya zao na kwamba elimu ya afya iendelee kutolewa kwa wanafunzi hao ili wavitumie vyoo hivyo kwa usafi.

"Msipofanya usafi kwenye masinki haya, yatabadilika rangi yatakuwa ya kijani au meusi au mekundu, na hapo ndio itakuwa mwanzo wa kuharibu afya zenu kwahiyo nawaombeni sana mjitahidi kuyasafisha," alisema Malima.

Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Joseph Kayombo, aliwataka walimu wa shule hiyo kuhakikisha wanasimamia utunzaji wa miundombinu ya shule hiyo vikiwemo vyoo ili kuhakikisha vinawasaidia kwa muda mrefu.

Aliwataka wananchi na wadau mbalimbali kuunga mkono juhudi za serikali kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki.

Kayombo alisema endapo mtu yeyote atakamatwa akifanya jambo lolote la kuharibu miundombinu ya shule, atachukuliwa hatua kali za kisheria kwa maelezo kuwa gharama kubwa zinatumika kujenga miundombinu hiyo.

UNICEF kupitia mradi wake wa SAWA, limekuwa likijenga miundombinu ya vyoo kwenye shule mbalimbali za msingi katika mikoa mbalimbali ambapo katika Mkoa wa Mbeya lilijenga katika shule mbalimbali za Halmashauri za Wilaya ya Mbeya na Chunya huku katika Mkoa wa Songwe wamejenga katika Mji wa Tunduma.



Kamishna wa Polisi Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Benedict Wakulyamba na Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, wakifunua pazia kuzindua Kituo cha Polisi Wanamaji cha Itungu, wilayani Kyela, mkoani Mbeya, baada ya kufanyiwa ukarabati na benki hiyo, kwa gharama zaidi ya Sh. milioni 48. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Shehena tumbaku yanaswa ikiuzwa nje ya mfumo rasmi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SHEHENA ya tumbaku imekamatwa ikiwa inauzwa nje ya mfumo rasmi wa uuzaji wa zao hilo wilayani Chunya.

Hali hiyo , ilisababisha Mkuu wa wilaya hiyo, Mayeka Simon Mayeka, kuamuru watu wawili ambao ni mkulima na mnunuzi wa tumbaku hiyo kuswekwa ndani.

Mayeka aliamuru watu hao kuwekwa ndani juzi, baada ya kukamatwa na tumbaku hiyo ya magendo akidai kuwa kitendo hicho ni sawa na uhujumu uchumi.

Akizungumza na wandishi wa Habari jana ofisini kwake, Mayeka alisema kuwa watu hao walikamatwa katika Kijiji cha Mtanila majira ya saa 2:00 usiku baada ya vyama vya msingi vya wakulima kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kufanya doria ya kudhibiti biashara ya magendo ya tumbaku.

Aliwataja watu waliokamatwa ni Twaha Edward ambaye ni mlanguzi wa tumbaku pamoja na Songora Rashid, mkulima na mwanachama wa Mtanila AMCOS aliyekuwa akiuza tumbaku hiyo.

"Kila msimu wa ununuzi wa tumbaku unapokaribia huwa kuna walanguzi wana tabia ya kupita majumbani kwa wakulima kununua tumbaku kinyemela... safari hii tuliamua kuweka mitego na kufanya doria kwa kutumia vyama vya ushirika wa wakulima na Polisi kudhibiti tabia hiyo na ndipo tumefanikiwa kuwakamata hawa watu," alisema Mayeka.

Alisema kuwa mkulima huyo alikopeshwa na chama cha msingi pembejeo kama vile mbolea na dawa za kuulia wadudu wa tumbaku, hivyo ana madeni ambayo hajalipa, lakini ameanza kuuza tumbaku yake na hivyo ni dhahiri kuwa baadaye hatoweza kulipa deni lake.

Alisema tabia hiyo imekuwa ikisababisha migogoro kwenye AMCOS nyingi na kusababisha Serikali kutumia muda mwingi kwenda kusuluhisha na wakati mwingine huwasababishia wakulima wenzake hasara kwa kulazimika kuwalipia madeni yao ya pembejeo.

Aidha, Mayeka alisema kuwa walanguzi hao wanaopita kwa wakulima wana tabia ya kununua tumbaku bora ya daraja la kwanza ambapo huwapunja wakulima kwa kununua kwa bei ndogo na hivyo kuwaongezea wakulima umasikini.

"Mfano mzuri ni tumbaku hii tuliyoikamata ikiuzwa na mkulima huyu kinyemela, tulipowaita watu wa bodi ya tumbaku wamefanya tathimini na kubaini kuwa kama ingeuzwa kwenye Amcos ina thamani ya Sh. 835,146, lakini cha kusikistisha mkulima huyu ameuza tumbaku hiyo kwa Sh. 118, 000," alisema Mayeka.

Mwakilishi wa Bodi ya Tumbaku wilayani Chunya, Faustine Mtweve, alisema kuwa tabia ya ulanguzi inaweza kusababisha malengo ya ukusanyaji wa tumbaku kwa mwaka huu wilayani Chunya yasifikiwe.

Alisema kwa msimu huu wa kilimo, malengo ni kukusanya kilo za tumbaku milioni 11. 44 kutoka kwa wakulima wapatao 400,000 wilayani Chunya pekee.

Alisema utoroshaji wa tumbaku ukiwepo huwenda malengo hayo yasifikiwe jambo ambalo litaathiri soko la tumbaku, mapato ya Serikali Kuu, Halmashauri, Amcoss na wakulima wenyewe.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alisema Tumbaku ni miongoni mwa mazao yanayotegemewa na Halmashauri yake katika kuingiza mapato yanayotumika kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi.

## Daladala zagoma, serikali yatupiwa lawama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHUGHULI za usafiri na usafirishaji katika Jiji la Mbeya zimekwama kwa siku ya pili mfululizo baada ya madereva wa magari ya kusafirisha abiria kugoma kufanya kazi wakidai kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza makubaliano ya kudhibiti pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la Bajaji.

Madereva hao wanadai kuwa waendesha bajaji wamekuwa wakiingilia njia zao na kuchukua abiria hali ambayo inawafanya wao washindwe kufikisha viwango walivyowekewa na wamiliki wa magari hayo.

Mgomo huo ambao ni wa pili tangu mwaka huu uanze umesababisha wananchi wakiwamo wanafunzi kupata shida ya usafiri na baadhi kulazimika kutembea kwa miguu na baadhi kutumia gharama kubwa kwenye usafiri wa bajaji na bodaboda kusafiri.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya madereva hao walisema wataendelea na mgomo huo mpaka serikali itakapotekeleza maazimio ya kuwawekea utaratibu mzuri waendesha bajaji na kuondoa mwingiliano wa njia.

Mmoja wa viongozi wa madereva hao, Raphael Simbeye, alisema kwenye kikao cha awali walikubaliana maazimio zaidi ya 10 lakini ni moja pekee ambalo limetekelezwa na mengine hayajatekelezwa hali ambayo inaendelea kuwaletea usumbufu.

Alisema azimio lililotekelezwa ni la kuwazuia madereva bajaji kuingia kwenye kituo cha daladala cha Kabwe na kuchukua abiria lakini mengine yote yakiwamo ya uzingatiaji wa sheria za usalama barabarani na kuondoka kwenye barabara ambazo zinatumiwa na daladala hayajatekelezwa.

Alisema baada ya kuona maazimio hayo hayatekelezwi, wamiliki wa daladala waliamua kusitisha huduma mpaka pale maazimio hayo yatakapokuwa yametekelezwa huku akidai kuwa wao wanafuata maelekezo ya wamiliki.

"Bajaji wanapita na kuchukua abiria hata maeneo ya 'wrong parking' (maeneo yasiyoruhusiwa) bila kukamatwa, lakini mimi wa daladala nikifanya hivyo wanakuja watu wa Jiji wananikamata na kunitoza faini za ajabu ajabu," alisema Simbeye.

Alisema wamekuwa wakitozwa faini mpaka ya Sh. 400,000, jambo ambalo linawaumiza na kuwafanya washindwe kufanya kazi yao kwa uhuru wakihofia kukamatwa na kutofikisha malengo ya mabosi.

Naye Anaceth Ambokile, dereva wa daladala za kutoka Uyole mpaka Stendi Kuu, alisema wanalazimishwa kupita katika barabara za kuzunguka eneo la Soweto na wasipotii wanakamatwa, lakini bajaji wanaruhusiwa kupita katikati na hawachukuliwi hatua yoyote.

Alisema kitendo hicho kinawafanya abiria wengi kukimbilia bajaji ili wafike haraka na hivyo kuifanya kazi yao kuwa ngumu tofauti na ilivyokuwa awali ambapo waendesha bajaji walikuwa wanafuata sheria kwa kupita kwenye njia zilizotengwa kwa ajili yao.



# Sheria, sera nzuri mazingira mazuri ya uwekezaji zaja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema inakusudia kuimarisha sera na sheria ambazo zitaweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuondoa urasimu.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti ya wizara hiyo.

Soraga alisema maeneo maalumu ya uwekezaji yaliyotengwa katika kisiwa cha Pemba huko Micheweni yataendelezwa na tayari zipo dalili nzuri za wawekezaji kuwekeza huko. Aliitaja miradi ya ujenzi wa viwanda vya kusarifu zao la mwani kuongeza thamani pamoja na viwanda vya uzalishaji wa mafuta ya mazao ya viungo ikiwamo mkaratusi vinatarajiwa kujengwa huko.

Alisema kwa sasa kazi kubwa inayofanywa na serikali ambayo ndiyo kipaumbele cha kwanza ni kusogeza huduma muhimu za miundombimu ukiwamo umeme, majisafi na salama na ujenzi wa barabara ambao upo katika hatua za mwisho.

"Mheshimiwa napenda kutoa ahadi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane kwamba maeneo huru yaliopo Pemba huko Micheweni ni moja ya kipaumbele cha serikali, na ndiyo maana tunasema serikali imekifanya kisiwa cha Pemba kuwa ukanda maalumu wa uwekezaji kwa sababu hizo, kuyatumia maeneo huru ya uchumi kwa uwekezaji," alisema. Aidha, Soraga alisema serikali imefungua milango ya kuwakaribisha wawekezaji zaidi pamoja na sekta binafsi katika uwekezaji wa miradi ya ujenzi wa bandari za mafuta na mizigo huko Mangapwani na Mpigaduri Mjini Unguja. Alisema serikali imejipambanua na kujenga uhusiano mzuri zaidi na sekta binafsi kwa ajili ya kujenga nchi na uchumi wa Zanzibar.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipitisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti hiyo ya Ofisi ya Rais, Kazi (Uchumi na Uwekezaji) kwa mwaka wa fedha 2012/2022 ambapo jumla ya Sh. bilioni 35 kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo zilipitishwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Saada Mkuya (katikati), akizungumza na watendaji wa wizara yake, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Rais Mwinyi mgeni rasmi Baraza la Eid

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Mufti Zanzibar imetangaza kuwa swala ya Eid El Fitri kitaifa mwaka huu itaswaliwa katika viwanja vya Maisara na Baraza la Eid litafanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakili Kikwajuni Mjini Zanzibar, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, atakuwa mgeni rasmi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu wa Mufti, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema iwapo kutanyesha mvua, swala hiyo itaswaliwa katika Msikiti mkubwa wa Jamiu Zinjibar uliopo Mazizini, pia itaswaliwa katika misikiti mengine.

Aliwakumbusha waumini wa dini ya Kiislamu kutekeleza ibada ya kutoa Zakatul Fitri kabla ya swala ya Eid ili kusafisha funga zao kutokana na mapungufu madogo na kuwasaidia waumini wenzao wasio na uwezo.

Sheikh Khalid alisema kuwa waumini wanaofuata utaratibu wa kuandama kwa mwezi sehemu yoyote duniani, sheria ya kiislamu inaruhusu kufungua, lakini asiwatangazie waumini wengine.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanaongeza ulinzi kwa watoto wao katika kipindi cha sikukuu ili kuwalinda na matukio mbalimbali yakiwamo ya udhalilishaji.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, alisema licha ya siku hiyo ni furaha kwa wananchi wote, lakini wasigeuze furaha hiyo kuwa sehemu ya kuwaacha watoto wakitembea ovyo mitaani, na wapo baadhi ya watu wenye nia mbaya wanaweza kusababisha madhara makubwa.

"Itakumbukwa kuwa katika miaka iliyopita kipindi kama hiki cha sikukuu huripotiwa kesi nyingi za udhalilishaji kwa wastani wa kesi tano kwa siku, ambapo watoto waliopo chini ya umri wa miaka 18 hutoroshwa ama kubakwa," alisema.

Hata hivyo mkurugenzi huyo alitoa wito kwa Jeshi la Polisi kuongeza kasi ya ulinzi zaidi katika maeneo mbalimbali ya viwanja vya kufurahishia watoto pamoja na kukagua magari yanayotoa huduma za abiria katika kipindi chote cha sikukuu.

# Waziri afunguka maeneo ya uwekezaji yalivyovamiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe Juma, amesema kuna uvamizi wa maeneo ya ardhi yaliyotengwa katika ukanda wa uwekezaji ambayo ni maeneo huru huko Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Aliyasema hayo wakati akitoa ufafanuzi na kujibu swali lililoulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa katika kuyahifadhi maeneo hayo na kuepuka na matukio ya uvamizi.

Waziri Pembe alisema eneo la ukanda wa uwekezaji maeneo huru ya Fumba limetengwa kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa viwanda vidogo na kati pamoja na miradi ya majengo ya makazi.

Alisema eneo la ukanda wa maeneo huru ukubwa wake ni 4,600 ambalo serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) wamekubali kufanya upembuzi yakinifu. Alisema upembuzi huo kwa kiasi kikubwa utasaidia kudhibiti matukio ya uvamizi wa ardhi, hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuweka matumizi sahihi ya ardhi katika uwekezaji.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba eneo la ukanda wa uwekezaji maeneo huru ya Fumba linavamiwa kwa kasi kubwa na chanzo ni kwamba eneo hilo halijapimwa na kufahamika matumizi yake sahihi," alisema.

Serikali ya Zanzibar chini ya Rais Mstaafu wa awamu ya tano, Dk. Salmin Amour Juma, ilitenga maeneo huru ya uchumi Fumba kwa upande wa Unguja na Micheweni kwa Pemba kwa lengo la kutumika uwekezaji wa miradi ya ujenzi wa viwanda.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa:-

1. Kiwanja cha Ndugu Julius Richard Mbaga kilichopo **VIKUGE-** Kibaha.
2. Kiwanja cha Ndugu Irene Matiku Nyamtonga Kilichopo Kitongoji cha Bwilingu – Chalinze.

Lengo ni kufidia/ kupunguza madeni ya mikopo wanayodaiwa. Minada itafanyika **Tarehe 21/05/2021**, mahali dhamana zilipo. Muda ni kuanzia saa nne Asubuhi.

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano fika ofisini kwetu Victoria 5th floor –DSM au Piga No. 0652113262**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD**, Sepco Na Champion tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa

| Mdaiwa/ mthamini | Dalali | Mahali | Tarehe mnada |
|---|---|---|---|
| Samira M. Mgombele (Mwinyimvua M. Lubawa) | **SEPCO** Debt Collection & Auctioneering Co. Ltd | Magomeni - Mtaa Mwinyimkuu | 28.05.2021 |
| Bernard Daud Nkeyemba | Championi Auction Mart | Kinzudi-Goba | 28/05/2021 |

Minada yote itafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO - 0715683777/0712670704**
**CHAMPION - 0769073836/0685108460**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SEKELA G MWAMBAJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1361-0131** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **SAMORA MACHEAL** mwaka **2015**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa MBS/RB/526/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.144/2021**

Ombi la **YUSTA LEINA MASAWE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **CANDIDUS NGALEKA NDUNGURU**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **16 / 06 / 2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 10 / 05 / 2021**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB:**
**+255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Museveni aapishwa kwa muhula wa sita

**Kampala,** UGANDA

RAIS Yoweri Museveni, amekula kiapo, jana kuliongoza taifa la Uganda, kwa muhula wa sita.

Sherehe za uapisho huo zilifanyika huku tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona ikichukuliwa.

Zaidi ya watu 4,000 wakiwamo viongozi kutoka kila pembe ya Bara la Afrika walihudhuria sherehe ya kuapishwa kwa Rais Museveni.

"Tumepambana na corona, hivyo sherehe hizi walioalikwa ni viongozi pekee," alisema Museveni katika ukurasa wake wa twitter.

Museveni ataiongoza Uganda kwa miaka mengine mitano, ikiwa ni muhula wake wa sita madarakani.

Aliingia madarakani Januari, mwaka 1986 kwa mapinduzi ya kijeshi, hadi utakapofika uchaguzi mwingine 2026 atakuwa madarakani kwa miaka 40, sawa na miongo minne. Wakati huo akiwa na umri wa miaka 81.

Alishinda uchaguzi Januari 14, mwaka huu kwa kuwabwaga wagombea wengine 10 katika nafasi ya urais kwa ushindi wa asilimia 58 ya kura zote.

Ijapokuwa wapinzani pamoja na waangalizi wa kimataifa na makundi ya haki za binadamu kudai kuwa uchaguzi huo, uliingiliwa na serikali ya Museveni na kuminya wagombea wa upinzani. Madai hayo hata hivyo yanakanushwa na serikali.

Usalama uliongezwa katika mji mkuu, Kampala, kabla ya kuapishwa kwake.

Wakuu wa nchi kadhaa tayari waliwasili kwenye sherehe hiyo, ikiwamo Burundi, Sudan Kusini na Somalia na Tanzania.

Siku ya Jumatatu, polisi walisema zaidi ya watu 40 walikamatwa kwa kupanga kuvuruga sherehe hiyo.

Askari waliizunguka nyumba ya Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, ambaye alikuwa mshindi wa pili wa uchaguzi. **BBC**

## Wabunge waitwa na spika Kenya shutuma za rushwa

**Nairobi,** KENYA

WABUNGE watatu wa Kenya, wameitwa na spika wa bunge baada ya kutoa madai kwamba wabunge walikuwa wamehongwa, ili kupitisha muswada wenye utata ambao utabadilisha katiba ya nchi hiyo kwa kiasi kikubwa.

Wabunge Moses Kuria, Ndidi Nyoro na Mohamed Ali, watafika mbele ya spika wa bunge baada ya kudai wenzao walipokea Dola 930 sawa na shilingi za Kenya 100,000 kila mmoja.

Fedha hizo zinadaiwa ni kwa ajili ya kupiga kura ya ndio kwa Muswada wa Marekebisho ya katiba maarufu kienyeji kama Jengo la Bridges Initiative (BBI).

Mpango huo umeungwa mkono na Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, ambao walisema itasaidia Kenya kukabiliana na mgawanyiko mkali wa kikabila, ambao ulizuka baada ya uchaguzi uliozozaniwa mwaka 2017/2018.

Ingawa wakosoaji wakiongozwa na Naibu Rais William Ruto, walidai ina maana tu ya kuunda nafasi za viongozi huku wakipuuza masuala ya haraka kama kupunguza umaskini na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira. **BBC**



Kenyatta



Ruto



Watu wakipita eneo lenye majengo ya makazi yaliyoharibiwa baada ya shambulio la anga la Israel na mjini Gaza, jana. **PICHA: AP**

# Zaidi ya Wapalestina 50 wauawa vurugu Gaza

**Gaza,** PALESTINA

WANAMGAMBO wa Hamas na wanajeshi wa Israel wameendelea kukabiliana Gaza na kwamba takribani watu 50 wameshauawa kufuatia machafuko ya siku kadhaa.

Hadi kufikia sasa Wapalestina zaidi ya 40 wameuawa na idadi kubwa ya wengine wakijeruhiwa kufuatia mashambulizi yanayofanywa na Israel hasa katika ukanda wa Gaza.

Majengo mawili ya ghorofa yaliporomoshwa na mashambulizi ya anga ya Israel huko Gaza.

Hamas ilifyatua zaidi ya roketi 200 kuelekea Israel na Waisreal watano waliuawa kufuatia mashambulizi hayo.

Israel ilifanya mamia ya mashambulizi kutoka angani kwenye ukanda huo wa Gaza jana, majira ya asubuhi kwa saa za Mashariki ya Kati huku wanamgambo wa kipalestina wa kundi la Hamas na makundi mengine katika ukanda huo nao wakifyatua roketi mji wa Tel Aviv na wa Kusini wa Beersheba.

Kufuatia hali hii ya machafuko Fatoue Bonsouda, mwendesha mashtaka mkuu wa Mahakama ya Kimataifa (ICC), inayoangalia kesi za uhalifu wa kivita alisema ana wasiwasi kwamba uhalifu wa kivita umefanywa na hasa kwa kutazama machafuko yanayotokea ukingo wa magharibi, ikiwamo Mashariki mwa Jerusalem pamoja na Gaza.

Kutokana na hali inayoendelea mwendesha mashtaka mkuu wa mahakama ya kimataifa inayoshughulikia uhalifu wa kivita ya ICC, alizungumzia wasiwasi wake, kwamba kuna uwezekano uhalifu umefanyika.

Bensouda aliandika ujumbe huo kwenye ukurasa wa Twitter jana, akiongeza kusema kwamba uchunguzi wa mahakama ya ICC utatazama pande zote na ushahidi unaohusika, kutathmini ikiwa kuna waliohusika na uhalifu, mujibu wa sheria za mahakama hiyo ya kimataifa.

Machi 3, mwaka huu, Bensouda raia wa Gambia alianzisha uchunguzi kamili kuhusu hali hiyo kwenye maeneo yaliyonyakuliwa na Israel, kitendo kilichoikasirisha Israel ambayo hata hivyo sio mwanachama wa ICC, tofauti na mamlaka ya Wapalestina.

Uchunguzi huo utalenga kutazama kilichotokea katika vita vya Gaza vya mwaka 2014 pia mauaji ya waandamanaji Wakipalestina mwaka 2018.

Jumuiya ya Kimataifa inashinikizwa kuitaka Israel ikomeshe matumizi ya nguvu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu, alisema, mashambulizi ya jeshi la Israel yanawaua Wapalestina huko Gaza.

"Tunalaani kila siku mashambulizi, lakini jumuiya ya ulimwengu wa kiislamu inatarajia sisi tuchukue hatua. Mashambulio aina hii yanapaswa kukomeshwa. Tunapaswa kulinda haki za Wapalestina kwa mujibu wa sheria ya kimataifa bila shaka," alisema Cavusoglu.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson kwenye ujumbe wake aliouandika kwenye ukurasa wa Twitter, alizitaka pande zote mbili Israel na Palestina kujizuia kutumia nguvu akisema Uingereza ina wasiwasi mkubwa na machafuko yanayoongezeka na idadi ya wanaouawa.

Kwa mujibu wa mjumbe wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mashariki ya Kati, Tor Wennesland, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, linatarajiwa kukutana kwa mara nyingine kuzungumzia mgogoro huu.

Kuna wasiwasi kwamba mgogoro huu unaweza kuelekea kwenye vita kamili na Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, alitangaza hali ya tahadhari katika mji wa Lod, unaokaliwa na jamii ya Wayahudi na Waarabu ambako polisi ilisema vurugu kubwa zilizuka katika baadhi ya sehemu za Waarabu. **DW**

# RONALDO KULAZIMISHA KUONDOKA JUVENTUS



**TURIN,** Iralia

CRISTIANO Ronaldo anaripotiwa atalazimisha uhamisho wake, kama klabu yake ya Juventus itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu ujao, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Wikiendi iliyopita Juventus waliruhusu kichapo cha mabao 3-0 wakiwa nyumbani dhidi ya wapinzani wao wa Serie A, AC Milan na wakajikuta wakishuka hadi nafasi ya tano katika msimamo wa ligi hiyo, wakati Napoli wakichukua nafasi yao kwenye nne bora.

Ronaldo anaweza kuikosa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza, kwa miaka 18 kama Juventus ikishindwa kumaliza ligi kwenye nafasi ya nne.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 36 ambaye ana mwaka mmoja ambao bado umesalia kwenye mkataba wake, atalazimisha klabu iweze kufanya uhamisho wake kwenda klabu ambayo inashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Juventus bado wana mechi dhidi ya Inter Milan, Sassuolo na Bologna kwenye mechi zao tatu za mwisho za Serie A msimu huu.

Mechi hizi ni muhimu kwao katika jaribio la kurejea kwenye nne bora ili wafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

# Tuchel kuongezwa miaka mitatu

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel yupo mbioni kupongezwa kwa kazi nzuri aliyoifanya tangu kukabidhiwa mikoba ya Frank Lampard pale Stamford Bridge kwa kupewa mkataba mpya.


Tuchel alipewa mkataba wa miezi 18 ukiwa na vipengele ambavyo inategemea mafanikio ya ndani ya uwanja.

Kati ya vipengele hivyo ilikuwa ni mafanikio ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuingia kwenye nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu England.

Kocha huyo amekuwa ni mkombozi kwa mashabiki wa Blues na amerejesha furaha na matumaini makubwa kwa mashabiki wa timu hiyo kwa muda mfupi alioiongoza timu hiyo baada ya Lampard kufutwa kazi pale darajani.

Chelsea ipo kwenye fainali mbili Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku ikiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa EPL mpaka sasa.

Imeripotiwa kuwa, uongozi wa klabu hiyo unatarajia kumwongezea mkataba Tuchel mwishoni mwa msimu huu wa miaka mitatu.





# Sporting wabeba ubingwa baada ya miaka 19

**LISBON,** Ureno

BAADA ya ukame wa miaka 19, klabu ya Sporting Lisbon wameibuka kidedea msimu huu kwa kubeba taji la Ligi Kuu Ureno.

Lisbon ambayo imetoa mastaa kama Cristiano Ronaldo, Luis Nani na Bruno Fernandez, imevunja utawala wa Benfica na FC Porto uliodumu kwa miaka 19 kwenye historia ya Primeira Liga.

Sporting wametwaa ubingwa huo baada ya kuwafunga Boavista 1-0, juzi Jumanne usiku.

Bao pekee lililofungwa na Paulinho limeifanya timu hiyo kukaa kileleni kwa tofauti ya pointi nane dhidi ya FC Porto wanaoshika nafasi ya pili zikiwa zimesalia mechi mbili msimu kumalizika.

Klabu hii inabeba ubingwa wa Primeira Liga ikiwa haijapoteza mchezo wowote mpaka sasa.

Huu ni mwendelezo wa mafanikio ya klabu hiyo ambayo mapema Januari, mwaka huu Sporting walitwaa taji lingine la Ureno.

Ni miaka mitatu tu imepita tangu mashabiki wa klabu hii wavamie uwanja na kuzua tafrani kwa wachezaji na wafanyakazi wa timu hiyo.

Tukio hili lilisababisha kocha wa wakati huo, Jorge Jesus, baadhi ya viongozi wakubwa pamoja na rais, Bruno de Carvalho wote kujiuzulu nafasi zao.

HABARI MICHEZO

# Garcia kusaini mitano Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa kulia wa Manchester City, Eric Garcia, anaripotiwa kuwa anasubiri tu kujiunga na Barcelona kwa mkataba wa miaka mitano.

Mkataba wa sasa wa Garcia unaisha mwishoni mwa mwezi ujao, na Pep Guardiola alithibitisha awali kuwa nyota huyu hajakubali kusaini mkataba mpya, hivyo atakuwa anaelekea Barcelona.


Tangu hapo, nyota huyo amekuwa akihusishwa na Barcelona, ambao walijaribu kumsajili katika hatua za mwisho za usajili wa Januari kabla ya dili hilo kufungwa.

Hata hivyo, taarifa zinasema kuwa Barcelona tayari wameshafanya makubaliano ya awali na Garcia ya mkataba wa miaka mitano, hadi 2026.

Hivyo nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, anatarajia kurejea Katalunya alikokulia.

Taarifa zaidi zinasema kuwa Rais Joan Laporta tayari ameshatoa ruksa ya nyota huyo kuwasili Barcelona kama mchezaji huru, na anaweza kuwa mchezaji rasmi mwisho wa msimu.

Garcia alitokea katika klabu ya Barcelona akijiboresha kufikia kikosi cha kwanza kabla ya kuondoka kuelekea Manchester City mwaka 2017.







# LINGARD KURUDI MAN UTD

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Jesse Lingard yupo mbioni kurejea Old Trafford baada ya kumaliza mkopo wake kwa wagonga nyundo wa London, West Ham United.

West Ham ipo kwenye wakati mgumu wa kumsajili moja kwa moja kutokana na thamani halisi ya nyota huyo inatajwa kufikia pauni milioni 21.

Lingard mwenye umri wa miaka 28 anataka mkataba wa miaka minne na mshahara usiopungua pauni 100,000 kwa wiki kiasi ambacho West Ham huenda ikawa mlima mrefu kwao licha ya kuwa na hitaji naye.

Lingard amebakiwa na mwaka moja katika mkataba wake na mashetani wekundu ambao ni wazi huenda kurejea kwake Old Trafford itakuwa ni sawa na kucheza karata isiyo tabirika.

Nyota huyo ambaye ni zao la United amecheza mechi tatu za msimu huu akiwa na klabu yake hiyo kabla ya kutolewa kwa mkopo kwenda West Ham ambapo katika mechi 13 alizocheza amefunga mabao tisa.

# *Joshua, Fury ulingoni Agosti*

**LONDON,** England

MABONDIA wa England, Anthony Joshua na Tyson Fury sasa watapanda ulingoni katika pambano la uzito wa juu kuwania mikanda mitatu nchini Saudi Arabia, kwa mujibu wa promota, Eddie Hearn.

Fury hajapanda ulingoni tangu alimpomchapa Deontay Wilder na kubeba mkanda wa WBC Februari, mwaka huu, huku Joshua atapanda ulingoni kutetea mikanda yake mitatu ya WBA, IBF na WBO ambayo aliichukua kwa ushindi dhidi ya Kubrat Pulev, Desemba, mwaka jana.

Kwa mujibu wa promota Hearn amenukuliwa na Sky Sports akisema pambano hilo la kukata na shoka litafanyika kati ya Agosti 7 au 14, mwaka huu.

Mabondia wote wawili wameonyesha furaha kwa sababu tayari "walitimiza kila ahadi zao" kwa pambano la Joshua dhidi ya Andy Ruiz mwaka 2019.

Bado hakuna tangazo rasmi ambalo limetolewa, lakini taarifa zimedokeza kwamba, mpango huo ulifanywa hivi karibuni.

Pambano hilo litakuwa la kwanza katika makubaliano ya mapigano mawili, na pambano la pili linatarajiwa kufanywa mwishoni mwa 2021. Imeripotiwa pia pambano hilo linaweza kutoa kiasi cha pauni milioni 500, huku Joshua na Fury wakikubali kugawana 50/50.

Fury hajapoteza katika mapambano 31 na kasoro yake pekee ni sare ya kutanisha dhidi ya Deontay Wilder mwaka 2018, pambano ambalo wengi waliona alishinda.

Wakati huo huo, Joshua ana rekodi ya 24-1, na kupoteza kwake kulikuwa kwa kushangaza mikononi mwa Ruiz mwaka 2019.



## DO ZA SOKA
## MA YA ULAYA



# GUARDIOLA AFUNGUKA CITY IKITWAA UBINGWA

### Asema ulikuwa ni msimu mgumu na wenye marufuku nyingi, lakini walipambana na kufikia...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema msimu huu umekuwa wa kipekee baada ya kunyanyua taji la Ligi Kuu England (EPL), juzi Jumanne.

**City ilishinda kwa mara ya tatu Kombe la Ligi Kuu England, kwa kipindi cha miaka minne, baada ya washindani wao wa karibu na wapinzani wa jiji moja, Manchester United kufungwa na Leicester City 2-1, Jumanne usiku.**

Kikosi hicho sasa kina alama 10 zaidi ya United ambao wapo nafasi ya pili huku wakiwa wamebakiwa na michezo mitatu peke yake.

Hii ni mara ya saba kwa City kushinda ubingwa wa England, na ni ubingwa wao wa tano ndani ya miaka tisa.

"Huu umekuwa msimu wa kipekee kabisa wa kuchukua taji la Ligi Kuu England," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari jana.

"Msimu huu ulikuwa mgumu. Tutaukumbuka daima msimu huu na jinsi tulivyoshinda. Ninajivunia kuwa kocha hapa na katika kundi la wachezaji hawa.

"Ni wachezaji wakipekee sana. Kushinda katika msimu huu, kukiwa na marufuku nyingi na changamoto tulizokabiliana nazo, lakini bado tukaendelea kufanya vizuri, ni jambo kubwa sana.

"Kila siku , wapo kwenye mapambano ya kufanikiwa, kujaribu kila siku kuwa bora zaidi. Tumekuwa mashujaa. "Nilikuwa Hispania, nikawa Ujerumani na ninaweza kusema hadi sasa kuwa hii ndio ligi ngumu. Hivyo ligi hii ina maana kubwa kwa kila mmoja."

Guardiola, mwenye umri wa miaka 50, ameshinda mataji nane ya ndani tangu ajiunge na City mwaka 2016. City ilikuwa na mwanya wa kushinda taji la EPL siku ya Jumamosi, lakini ilifungwa na Chelsea kwa mabao 2-1.

Hata hivyo, Leicester waliimaliza kazi yao kwa kuifunga United 2-1 katika Uwanja wao wa Old Trafford.

Ni ubingwa wa sita ambao umeamuliwa kwenye uwanja Old Trafford - ikiwa ni idadi kubwa zaidi kuliko uwanja mwingine wowote - na kati ya mara hizo sita United imenyakua ubingwa mara tatu na mara tatu zilizosalia ukienda kwengine, ikiwamo msimu huu.

Huu ni ubingwa wa pili kwa City ndani ya kipindi cha wiki mbili baada ya kuifunga Tottenham Hotspur katika fainali ya Kombe la Carabao.

City pia wameingia katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza baada ya kuwafunga mabingwa wa Ufaransa Paris St-Germain wiki iliyopita.

Tangu iliponunuliwa na matajiri kutoka Abu Dhabi mwaka 2008, City imeshanyakua makombe 12.

Wanatarajia kupatiwa kombe lao katika mechi ya mwisho dhidi ya Everton Mei 23, mwaka huu mbele ya mashabiki 10,000.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMGANDA KANE

MANCHESTER United bado wanaendeleza juhudi za kumnasa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

### DEMBELE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL wanajipanga kumsajili mshambuliaji Mfaransa, Moussa Dembele. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 yuko Atletico Madrid kwa mkopo akitokea Lyon. ***(Telegraph)***

### ROMA YAMTAKA WHITE

AS Roma wamejiunga katika kinyang'anyiro cha usajili wa mlinzi wa Brighton, Ben White mwenye umri wa miaka 23, kwa maelekezo ya kocha wao mpya, Jose Mourinho. ***(Sun)***

### TUCHEL MAMBO SAFI

CHELSEA wanatarajiwa kumpatia kocha wao, Thomas Tuchel, mkataba mpya mpya wa miaka mitatu baada ya msimu huu kufikia tamati. ***(Mail)***

### GARCIA SAFI BARCA

BARCELONA wameafikiana na Manchester City kumsajili mlinzi wa Hispania, Eric Garcia, mwenye umri wa miaka 20, kwa uhamisho huru. ***(Goal)***

### GIROUD AGEUKA LULU

INTER Milan na Lazio wanamnyatia mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34. ***(Calciomercato)***

### ROMERO AMFUATA MOURINHO

JOSE Mourinho ana matumaini ya kuungana tena na kipa wa Manchester United na Argentina, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 34, atakapochukua rasmi usukani kama kocha wa Roma. ***(Express)***

### HEATON AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United wanakaribia kumsajili golikipa, Aston Villa, Tom Heaton mwenye umri wa miaka 35, kuchukua nafasi ya Sergio Romero. ***(Sun)***

### AURIER KUTUA MILAN

AC Milan wanamtaka mlinzi wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Serge Aurier mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

### MADRID SOKONI

REAL Madrid pia wamefanya mawasiliano na Tottenham juu ya Serge Aurier, ambaye mkataba wake Spurs unakamilika mwaka 2022. ***(Foot Mercato)***

### LEEDS YAIONYA LIVERPOOL

LEEDS United wamewaambia wapinzani wao katika Ligi Kuu England, Liverpool kusahau kuhusu kumsajili mshambuliaji wao, Patrick Bamford mwenye umri wa miaka 27. ***(Star)***

## HABARI MICHEZO

# Asukile amvuruga Pawasa ufukweni

Na Saada Akida

HATIMA ya mchezaji wa Tanzania Prisons, Benjamin Asukile kutumikia Timu ya Taifa ya Ufukweni iko chini ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), wakati kikosi hicho kikijiandaa kuelekea Senegal katika fainali za Kombe la Mataifa Afrika (BSAFCON 2021), imeelezwa.

Kamati ya Saa 72 ya TFF ilitangaza kumfungia Asukile mechi tano pamoja na kulipa faini ya Sh. 500,000 baada ya kubainika kufanya makosa katika mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo ya Tanzania, Boniface Pawasa alisema amepokea kwa masikitiko taarifa za kufungiwa kwa nyota huyo ambaye yuko katika mipango yake kuelekea michuano hiyo.

Pawasa alisema bado mchezaji huyo yuko kambini na sasa anasubiri kupata mwongozo kuhusiana na hatima yake kutoka kwenye mamlaka zinazosimamia mpira hapa nchini.

"Nimesoma vizuri taarifa na adhabu ya mchezaji huyo, amezuiliwa kucheza mechi tano za mashindano yanayosimamiwa na TFF na sisi tunaenda kushiriki michuano inayosimamiwa na CAF (Shirikisho la Soka Tanzania), kwa mwongozo wa TFF, tunasubiri maelekezo."

"Tumeomba ufafanuzi juu ya kuhusu suala hili, kama adhabu hiyo itamgusa pia katika majukumu ya timu ya taifa, hawezi kushiriki michuano hiyo, tutamwondoa kikosini na kurejea nyumbani kutumikia adhabu yake," alisema Pawassa.

Aliongeza maandalizi ya timu hiyo yanaendelea vizuri na wamepata mechi tatu za kirafiki ambapo wamecheza mechi mbili dhidi ya klabu mbili za visiwani Zanzibar na nyingine walipambana na Kombaini ya Timu ya Taifa ya ufukweni ya visiwani humo.

"Mechi yetu ya mwisho tutacheza kesho (leo), hiyo itanipa mwanga wa kuona mapungufu na kufanyia kazi kabla ya kuanza safari ya kuelekea Senegal kwa ajili ya kushiriki michuano hiyo ya AFCON," alisema Pawasa.

Alisema anaamini kikosi chake kitakwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika fainali hizo na hatimaye kupata tiketi ya kushiriki michuano ya dunia itakayochezwa nchini Urusi.

# MBEYA KWANZA YAANZA VIJEMBE MAPEMA BARA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, klabu ya Mbeya Kwanza imeanza kutoa maneno ya kutamba dhidi ya timu nyingine zinazoshiriki ligi hiyo ya juu nchini na kuanzisha 'gumzo' katika mitandao ya kijamii na vipindi mbalimbali vya michezo hapa nchini.

**Katika ukurasa wake rasmi wa klabu hiyo wameandika kijembe ikiuliza "tuambieni anayewaonea ni nani?"**

Tafsiri ya wengi baada ya kusoma maneno hayo ni kwamba klabu hiyo ambayo itaanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao wa 2021/22 inauliza timu ipi ni tishio na inatoa dozi ili wao wajipange kulipiza kisasi watakapokutana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Mbeya (MREFA), Lucas Kubaja, ameeleza furaha yake ya kupata timu nyingine ya jiji hilo kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kubaja alisema wanajivunia mafanikio ya Mbeya Kwanza kwa sababu watapata nafasi ya kuutangaza mkoa wao kila watakapokwenda kucheza ugenini huku michezo zaidi ya ligi hiyo ikiongezeka katika mkoa wao.

"Nichukue nafasi hii kama Katibu Mkuu kwa niaba ya uongozi kuipongeza klabu ya Mbeya Kwanza kwa kupanda Ligi Kuu, hii ni fahari kwa mkoa mzima, kwa maana hiyo msimu ujao watu wa Mbeya burudani zitakuwa nyingi tu, maana tuna Mbeya Kwanza, Mbeya City, Ihefu na Tanzania Prisons, nina uhakika zote zitakuwapo," alisema Kubaja.

Kuhusu Mbeya Kwanza kutumia Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani katika mechi zake za nyumbani msimu huu, alisema pamoja na uamuzi wa kuhamisha kituo, lakini bado klabu hiyo inatambulika ni wenyeji wa Mbeya na wana mawasiliano ya karibu katika kukamilisha taratibu mbalimbali za utawala.

"Tulikuwa na mawasiliano nao ya karibu, kwa hiyo haina tatizo kuwa msimu ujao tutakuwa nao huku Mbeya," Kubaja alisema.

Timu hiyo ilikuwa ya kwanza kupanda daraja baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya African Sports ya jijini Tanga katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani, bao pekee lililofungwa na Willy Edgar dakika ya 75.

Ni ushindi ambao uliwafanya kufikisha pointi 38 na kuwa kinara wa Kundi A huku ikiwaacha African Sports kwenye nafasi ya pili wakiwa na pointi 28.

Mbeya Kwanza ni timu iliyoanzishwa mwaka 2012 ikiitwa Coca Cola Kwanza, lakini ilipofika mwaka 2014 ilibadilishwa na kuitwa Mbeya Warriors wakati huo ikishiriki Ligi ya Mabingwa Ngazi ya Mkoa.



Wachezaji wa Azam FC wakiwa katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# *Kagera Sugar yatangaza vita Kaitaba*

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo dhidi ya Mwadui FC kimempa matumaini makubwa ya kuendelea kubakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaelekea ukingoni.

Baraza alisema lengo lake ni kuona kikosi hicho kinavuna pointi zote tisa kwenye uwanja wa nyumbani wa Kaitaba na kujiondoa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Kocha huyo huo ni ushindi wa kwanza tangu alipochukuwa majukumu ya kukinoa kikosi cha timu hiyo na bado wanapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwenye michezo iliyobakia.

Alizitaja mechi zilizobakia watakazocheza nyumbani ni dhidi ya Ruvu Shooting itakayofanyika Mei 17, mwaka huu halafu wataikaribisha Ihefu SC na baadaye Tanzania Prisons.

"Tumejipanga kuhakikisha tunapata pointi tatu katika kila mechi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuendelea kucheza ligi kwa msimu ujao. Ligi imekuwa na ushindani mkubwa sana na kila mmoja anahitaji kupata pointi tatu, kwa sababu kuna watu wanahitaji ubingwa na wengine kujinasua kushuka daraja kama ilivyo kwetu."

"Tuko katika hali mbaya nina imani kwa kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wangu katika mchezo wetu dhidi ya Mwadui, tena ugenini, dalili za kubakiza pointi tisa nyumbani zitatimia," alisema Baraza.

Kagera Sugar yenye pointi 30 iko katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kucheza michezo 29 wakati vinara wa ligi hiyo ni mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 61.

# Michezo

Alhamisi Mei 13, 2021

Nipashe




Guardiola afunguka City ikitwaa ubingwa UKURASA 22



Magolikipa wa Simba kutoka kushoto ni Ally Salim, Aishi Manula na Beno Kakolanya wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali dhidi ya wenyeji Kaizer Chiefs itakayochezwa keshokutwa Jumamosi kwenye Uwanja wa FNB jijini Johannesburg, Afrika Kusini. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA SC YATAMBA KUISHANGAZA AFRIKA

## ● ● ● Ni katika mechi dhidi ya Kaizer Chiefs, lakini Gomes pia aitolea jicho FA...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha wawakilishi wa Tanzania kikiendelea vyema na mazoezi huko jijini Johannesburg, Afrika Kusini kwa ajili ya kuwakabili Kaizer Chiefs, Kocha Mkuu wa Simba Didier Gomes amesema licha ya mechi za Kombe la FA kuwa ngumu, timu yake imejipanga kutetea ubingwa wa michuano hiyo wanaoushikilia.

**Simba itaikaribisha Dodoma Jiji FC katika mechi ya hatua ya robo fainali itakayochezwa kati ya Mei 25 na 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam huku keshokutwa ikishuka ugenini kuwakabili Kaizer Chiefs katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Mechi kati ya Kaizer Chiefs dhidi ya Simba itachezwa kwenye Uwanja wa FNB kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Gomes aliliambia gazeti hili amefurahishwa na ratiba ya mechi za michuano hiyo na kuitaja Dodoma Jiji ni moja ya timu nzuri hapa nchini, lakini amesisitiza Simba wanalihitaji kombe hilo.

Kocha huyo alisema amefuatilia droo hiyo na wamepangwa kucheza dhidi ya Dodoma Jiji ambayo ni timu nzuri na aliiona kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ilipocheza na Simba.

"Haitokuwa mechi rahisi. Dodoma Jiji ni timu nzuri, nimecheza nayo. Siyo rahisi kuifunga, na kama tukipita hapo nafikiri kwa kiasi kikubwa tutakutana na Azam. Nayo ni timu nzuri na ngumu, niliiona ilipocheza na Yanga na kushinda bao 1-0, lakini nawaamini sana wachezaji wangu. Simba kwa sasa ni timu nzuri na ushahidi kwenye mechi ya FA iliyocheza dhidi ya Kagera Sugar. Ilikuwa mechi nzuri sana," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanahitaji kulichukua kombe hilo ili kuendeleza ubora waliouonyesha msimu huu na anaamini uwezo wa kulichukua wanao.

"Ni droo ngumu lakini tunataka kushinda kila kitu, kila kombe msimu huu. Ni muhimu kwetu kama tutashinda Kombe la FA, tutakuwa tumefanya kazi nzuri sana na nawaamini vijana wangu," Gomes alisema.

Kuelekea mchezo wa keshokutwa, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema kikosi chao kiko imara na kila mchezaji ana morali nzuri.

Manara alisema Simba inauwezo wa kufanya vizuri katika mchezo huo na wanaamini wanaweza kupata ushindi ugenini.

"Hatuna majeruhi, hiyo ni faraja kwetu, tuko tayari kwa ajili ya mchezo wa Jumamosi, tuliwasili hapa Johannesburg salama, maandalizi yako vizuri, timu yetu iliyotangulia imetuandalia mapokezi mazuri, balozi ametupokea vizuri... tunamwomba Mwenyezi Mungu Inshaallah hadi siku ya Jumamosi tusiwe na majeruhi yoyote, tunaweza huenda tukaishangaza Afrika kwa kupata matokeo ugenini," alisema Manara.

Baada ya mchezo huo wa kwanza, Simba itarejea nchini tayari kuwakaribisha Kaizer Chiefs katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Mei 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Yanga yasaka makali Mtwara

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kimeamua kuweka kambi ya muda mkoani Mtwara kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya kuivaa Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo imesema uamuzi wa kuweka kambi Mtwara umetokana na mapendekezo yaliyotolewa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nassredine Nabi ambaye alihitaji sehemu yenye utulivu zaidi.

"Tumefika Mtwara salama, Kocha Mkuu amehitaji kukaa mjini hapa kwa siku mbili ili kuendelea na programu yake, na Ijumaa ndio tutakwenda Lindi," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza wakiwa Mtwara wanahitaji kujiimarisha ili kusaka matokeo chanya katika mechi hiyo ya kiporo ambayo wanahitaji ushindi na kuendelea na mbio za kuwania taji la ubingwa wa msimu huu.

"Kocha Nabi amepata taarifa za nyuma kuhusu wapinzani wetu, ndio sababu ametaka kupata nafasi ya kuandaa timu yake vyema ikiwamo kufanya mazungumzo maalumu na wachezaji ambayo yatajenga kisaikolojia, lakini kuwaandaa kimbinu."

"Namungo ni timu imara, hatutawabeza wapinzani wetu, tunaimani mchezo huo hautakuwa rahisi kwa sababu ya maandalizi ya kikosi tulichonacho pamoja na mbinu za kocha, kikubwa ambacho tunahitaji kupata ni matokeo chanya," aliongeza.

Alisema wachezaji wako tayari kupambana na kutafuta ushindi dhidi ya Namungo FC, licha ya timu hiyo kuonyesha ushindani katika kila mechi wanayokutana.

"Namungo FC wamekuwa wagumu sana kwetu tangu wamepanda Ligi Kuu, imekuwa ikitusumbua nyumbani na ugenini, sasa tumejipanga vizuri kwa ajili ya kutafuta pointi tatu katika mchezo huo," aliongeza kiongozi huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >